**Samia** aifumua RITA, aanza ziara Mwanza

UKURASA 3



**ACT** - Wazalendo yakosoa machinga kutolewa mjini

UKURASA 3


NIPASHE JUMATATU JUNI 12, 2023
Nipashe
Spotika
HAZARD NA FUNGU LA KUKOSA REAL MADRID UK. 12-13
ISIKUPITE
BEKI Mwingereza Harry Maguire anaweza akaikosesha nafasi klabu yake ya Manchester United kumsajili beki wa kati wa Napoli raia wa Korea Kusini, Kim Min-jae (26), kama Mwingereza huyo atakataa ombi la klabu hiyo la kumtaka aondoke Old Trafford, mchezaji huyo tayari ameonyeshwa mlango wa kutokea ili kuipa nafasi klabu hiyo kusajili beki mwingine.
ZAHA
WACHEZAJI 6 HURU AMBAO MAN UNITED INAWEZA KUWAPATA

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Juni 12, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • Na. 0581339

The ... igital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




# Makundi CCM

• **Uongozi** wa juu wabaini kuwapo 'vibaraka wa upinzani'... *Endelea ukurasa wa 2*




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (wa tatu kulia) akipokea gawio la serikali la Sh. bilioni 24.6 kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay (wa pili kushoto). Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Abdulmajid Nsekela (kushoto), Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Natu El- Maamry Mwamba (wa pili kulia). Habari Uk. 7. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## 188,000 wachaguliwa kidato cha V, ualimu na vyuo ufundi

UKURASA 2



RIPOTI YA UCHUNGUZI

# Hivi ndivyo ulivyo unyama askari-pori kwa wanakijiji

• **Hofu** yatanda, wenyeji waibua yasiyotajwa... *Endelea ukurasa 4*

**MICHEZO** **NBC YAIPONGEZA YANGA UBINGWA** UK.23 **KATUNI** UK.6

# 188,000 wachaguliwa kidato cha V, ualimu, vyuo ufundi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, ametangaza wanafunzi 188,128 kuchaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano, vyuo vya ualimu na vyuo vya elimu ya mafunzo ya ufundi Tanzania Bara kwa mwaka wa masomo 2023.

Wanafunzi hao ni kati ya 192,348 waliopata ufaulu wa daraja la kwanza hadi la tatu kwenye matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka jana.

Pia wanatakiwa kuripoti shuleni kuanzia Agosti 13 hadi 31, mwaka huu kwa ajili ya kuanza ratiba ya masomo yao.

Akizungumza na waandishi wa habari, Waziri Kairuki alisema kati ya wanafunzi waliopangiwa shule na vyuo, wasichana ni 84,509 na wavulana 103,619.

"Idadi hii inajumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalum 490 ambao wasichana ni 218 na wavulana ni 272.

"Wanafunzi 129,830 wakiwamo wasichana 66,343 na wavulana 63,487 sawa na asilimia 69 ya wenye sifa ndiyo waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano kwenye shule 540," alisema Kairuki.

Aidha, alisema wanafunzi 1,878 wakiwamo wasichana 1,097 na wavulana 781, wamepangiwa katika shule za sekondari maalum Kilakala, Mzumbe, Ilboru, Kisimiri, Msalato, Kibaha, Tabora Boys na Tabora Girls.

Wanafunzi 122,908 wakiwamo wasichana 62,731 na wavulana 60,177 wamepangiwa shule 519 za sekondari za bweni za kitaifa za kidato cha tano.

Alisema wanafunzi 5,044 wakiwamo wasichana 2,515 na wavulana 2,529 wamepangiwa katika shule 11 za sekondari za kutwa za kidato cha tano.

Kairuki alisema kwa upande wa vyuo, wanafunzi 58,298 wakiwamo wasichana 18,166 na wavulana 40,132 sawa na asilimia 31, wamepangiwa kujiunga kwenye kozi mbalimbali za stashahada katika vyuo vya kati vinavyosimamiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET).

Pia wanafunzi 1,645 wakiwamo wasichana 646 na wavulana 999 wamechaguliwa kujiunga na vyuo vya ualimu ngazi ya stashahada ya sayansi, hesabu na TEHAMA.

Alisema waliochaguliwa kujiunga na fani mbalimbali kwenye vyuo vya ufundi ni wanafunzi 1,877 wakiwamo wasichana 757 na wavulana 1,120.

Vyuo hivyo ni Chuo cha Ufundi cha Arusha (ATC), Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya-MUST na Chuo cha Usimamizi na Maendeleo ya Maji (WDMI).

Kairuki alisema waliochaguliwa kujiunga na vyuo vya afya ngazi ya stashahada ni wanafunzi 1,842 wakiwamo wasichana 943 na wavulana 899.

Kadhalika, waliochaguliwa kujiunga kwenye kozi mbalimbali za kilimo, ufugaji, utawala, biashara na zingine za stashahada katika vyuo vya kati ni wanafunzi 52,934 wakiwamo wasichana 15,820 na wavulana 37,114.

"Wanafunzi wote waliopangwa kujiunga na kidato cha tano kwa mwaka, 2023 wanapaswa kuanza kuripoti shuleni kuanzia Agosti 13, 2023 na siku ya mwisho ya kuripoti ni Agosti 31, mwaka huu.

"Fomu za maelezo ya mahitaji ya kujiunga na kidato cha tano kwa shule zote za kidato cha tano zinapatikana kwenye tovuti ya OR-TAMISEMI kupitia kiunganishi cha www.tamisemi.go.tz"alisema

Kairuki alisema kwa kuzingatia ufaulu na nafasi zilizopo, hakutakuwa na fursa ya kufanya mabadiliko yoyote ya shule kutokana na ukosefu wa nafasi.

Aliwaagiza wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha azma ya serikali ya kuwa na shule za sekondari za kidato cha tano katika kila tarafa inatekelezwa ili kuwezesha wanafunzi wote wanaofaulu kidato cha nne kupata nafasi ya kuendelea na masomo ya kidato cha tano na sita.

Aliwataka viongozi hao kuhakikisha wanaendelea na upanuzi na ujenzi wa shule mpya za kidato cha tano na sita na kuongeza tahasusi za masomo ya sayansi.

"Mikoa ihakikishe inakuwa na tahasusi zote za msingi katika shule zake ili kuwapunguzia wazazi au walezi gharama za usafiri kwenda shule za mbali," alisisitiza Kairuki.



Waziri wa Nishati, January Makamba (katikati), akimsikiliza Mkuu wa Kanda wa Benki ya Exim Tanzania, Elizabeth Mayengo (kulia), akielezea kuhusu huduma za kibenki zinazotolewa na benki hiyo mahususi kwa ajili ya wanawake na mchango wake katika kuunga mkono jitihada za serikali kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia. Waziri Makamba aliongoza uzinduzi wa mafunzo ya namna ya kutumia nishati mbadala kwa mamalishe na vijana yaliyoandaliwa na Mtandao wa Uwezeshaji Wanawake Tanzania (TAWEN) mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi akemea makundi CCM

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewakemea wana-CCM wanaoendekeza makundi huku akiwataka kuelekeza nguvu kukijenga chama kwa uchaguzi wa 2025.

Amesema Tanzania, haiwezi kuendeshwa na chama kingine cha siasa isipokuwa CCM na kuwa ni vyema viongozi wakahakikisha wanaendelea kuwatumikia wananchi ili kujenga imani kwao na chama.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana wakati akizungumza na mabalozi, wajumbe wa mabalozi na wajumbe wa Halmashauri ya CCM, Mkoa wa Kaskazini Unguja katika kuhitimisha ziara za kichama Kisiwa cha Unguja.

Alisema miongoni mwa njia zitakazo kiwezesha chama hicho kusonga mbele kushika dola ni kuwa wamoja na kuondoa makundi.

Dk. Mwinyi alisema ataendelea kufanya kazi kwa kadri ya uwezo wake lengo ni kukiendeleza kukipa nguvu chama hicho, huku akiwasisitiza viongozi na wanachama kuendeleza umoja uliopo ndani ya chama.

Alisema baada ya uchaguzi wa chama kumalizika zipo kasoro zilijitokeza kutokana na makundi na kusisitiza ni vyema kuyaacha makundi hayo ili kukipa ushindi chama wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

"Wanachama wenzangu naomba tuendelee kushikamana zaidi kwa maslahi ya chama chetu, tusivurugwe na kuendekeza makundi ya wakati wa uchaguzi, tayari viongozi wamepatikana na uchaguzi wa chama umekwisha na sasa tujielekeze katika uchaguzi wa 2025," alisema.

"Tunajua kuwa yapo makundi ndani ya chama baada ya kumalizika kwa chaguzi maana kila mmoja alikuwa na mgombea wake sasa uchaguzi umekwisha tuungane pamoja na tuvunje kambi zetu na tuwe nyuma ya wale waliochaguliwa," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema kazi ya kwanza ya chama cha siasa ni kushika dola, wana CCM wanawajibu wa kujiandaa kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 ili CCM iendelea kushika dola.

"Kuna watu wameanza kuwa vibaraka wa wapinzani kwa kupotosha na kutoa kauli zisizofaa kwa wanachama na wananchi, kama mtu hakitaki chama aondoke tu, lakini asituharibie chama chetu," alisisitiza Dk. Mwinyi.

Aliwataka viongozi hao kuanza kuhakiki daftari la wapigakura, ili kujua wapigakura pamoja na kuwahimiza wanachama kulipa ada za uanachama na kuacha kusubiri kipindi cha uchaguzi na kulipiwa na wagombea.

Kuhusu huduma za afya, Dk. Mwinyi alisema anatarajia kujenga hospitali mbili kubwa za utoaji wa huduma za wazazi, ili kurahisisha huduma kwa wajawazito wanaokwenda kujifungua.

Alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa Ilani ya CCM na lengo lake kuu ni kuendelea kutoa huduma nzuri kwa wananchi wa visiwani humo.

Kwa mujibu wa Dk. Mwinyi, sera ya utoaji huduma bure itaendelea kuwapo ingawa kumekuwapo kwa maboresho mbalimbali, lengo ni kuwapatia huduma bora wananchi wa visiwa hivyo.

Kuhusu kujiwekeza kiuchumi, Dk. Mwinyi alisema, ni wajibu wa viongozi kujenga uchumi katika chama na kuwa na majengo yenye hadhi na vitendea kazi na vyombo vya usafiri pamoja na kuwatizama watendaji wao katika maslahi yao.

Naibu Katibu wa Chama cha CCM Zanzibar, Dk. Mohamed Said Mohamed, maarufu Dimwa, alisema CCM itaendelea kuisimamia serikali ili kufikisha maendeleo kwa wananchi wote, ikiwamo miradi inayotekelezwa na kauli zinakuwa moja kati ya serikali na chama.

Alisema serikali imeshakamilisha ujenzi wa madarasa 158 na zinaendelea kujengwa shule tano za ghorofa za kisasa ndani ya mkoa huo kuimarisha sekta ya elimu.

Kadhalika, CCM itaendelea kuzisimamia na kuelekeza serikali, kutoa huduma bora na zenye viwango kwa jamii.

"CCM ndiyo chama pekee chenye kuleta mabadiliko ya kweli ya kimaendeleo kwa wananchi wote wa visiwa vya Zanzibar, hivyo tuendelee kuunga mkono," alisema Dk. Dimwa.

Katibu wa Kamati Maalum ya NEC, Idara ya Itikadi na Uenezi CCM Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis, alisema ndani ya mkoa huo kinajengwa kiwanda cha kusindika samaki kwa ajili ya kuongeza thamani mazao ya bahari.

Alisema kupitia Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi (ZIPA), jumla ya miradi 230 imesajiliwa asilimia 60 ya miradi hiyo inatekelezwa Kaskazini Unguja kwa lengo la kuongeza fursa za uwekezaji.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema Dk.Mwinyi, ameendelea kutekeleza Ilani kwa ufanisi katika eneo la miundombinu kwa kujenga barabara za viwango vya lami katika mkoa huo.

Mkoa huo una mtandao wa barabara wenye urefu wa zaidi ya kilomita 45.2 ambazo nyingi ni za kiwango cha lami.

Akizungumzia utekelezaji wa Ilani, Waziri wa Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wanawake, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, alimpongeza Dk. Mwinyi kwa kuongeza pensheni ya wazee kutoka 20,000 hadi 50,000 kwa mwezi.

Alisema kwa sasa vikundi mbalimbali vya wanawake na makundi mengine yameendelea kupata mikopo na wamejenga jengo la kisasa kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake.

HABARI KITAIFA

# Rais Samia aifumua RITA

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameteua Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) kwa kumteua Frank Kanyusi, kuwa Kabidhi Wasii Mkuu ambaye kabla ya uteuzi huo alikuwa Mwanasheria Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara.

Frank anachukua nafasi ya Angela Anatory, ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Pia amemteua Irene Lesulie kuwa Naibu Kabidhi Wasii Mkuu, ambaye kabla alikuwa Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Mashauri ya Kimataifa, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Lesulie anachukua nafasi ya Lina Sanga, ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, uteuzi huo unaanza Juni 8, mwaka huu.

Katika hatua nyingine, Rais Samia leo anatarajiwa kuanza ziara ya kikazi ya siku tatu mkoani Mwanza kwa ajili ya kukagua miradi ya kimkakati, kuzungumza na wananchi na kufungua Tamasha la Kitamaduni la Bulabo.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa Rais Samia atawasili leo saa 12 jioni.Alibainisha kuwa kesho atashiriki ufunguzi wa Tamasha la Utamaduni la Bulabo litakalofanyika wilayani Magu, likihudhuriwa na machifu mbalimbali wa ndani na nje ya mikoa ya Kanda ya Ziwa. "Ikumbukwe katika tamasha kama hilo ndiko alipotunikiwa na machifu nchini kuwa kiongozi wao na kumuita Chifu Hangaya hivyo wananchi wote wanakaribishwa kushiriki katika tamasha hilo la kihistoria," alisema Makalla.

Alisema kuwa Jumatano atatembelea na kukagua miradi ya kimkakati mitatu ya Daraja la JPM, Hoteli ya PSSSF na meli kubwa ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu.

# ACT-Wazalendo yakosoa machinga kutolewa mjini

**Na Julieth Mkireri,** MWANZA

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema hakikubaliani na uamuzi wa kuwaondoa wafanyabiashara wadogo (machinga) katikati ya mji badala yake serikali inatakiwa kutenga maeneo ambayo yana watu wengi kwa ajili ya kundi hilo kufanya biashara.

Katika mkutano uliofanyika jijini Mwanza jana, Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe, alisema kuwaondoa katikati ya miji machinga kumesababisha baadhi yao mitaji kuisha na wengine kukwama kulipa mikopo, hivyo kuzalisha umaskini kwa kundi hilo.

"Kwa hiyo, pendekezo letu ACT-Wazalendo ni kwamba miji inaweza kutumika na wote kwa maslahi ya wote na ni lazima machinga ya Mwanza watengewe eneo katikati ya mji," alisema.

Zitto pia alisema chama hicho kimepokea malalamiko ya kuwapo 'utitiri' wa tozo katika uvuvi, jambo ambalo linachangia kuwarudisha wavuvi katika umaskini.

"Mkulima akiwa na trekta, hana leseni hatozwi. Mvuvi akiwa na boti au mtumbwi, wanamtoza leseni wakati ndio chombo chake cha uzalishaji. Haya yote tunapendekeza yaondolewe ili mvuvi afanye shughuli zake na kuondoka katika umaskini," alisema.

Kuhusu sakata la bandari, Zitto alisema ni wajibu wa serikali kutoa ufafanuzi kwa wananchi baada ya Bunge kutekeleza wajibu wake kwa kupitisha azimio. Alisema ACT-Wazalendo inaangalia namna ya kusukuma ajenda ya kurekebisha vifungu vya mkataba ambavyo wanaona vinahitaji kurekebishwa ikiwamo kuweka wazi bandari zitakazohusika na ambazo hazitahusika katika mkataba huo.

Alisema sheria za nchi zinataka mtu yeyote anayeendesha bandari ni lazima awe na hisa za wazawa, hivyo chama chao kinapendekeza kampuni hiyo ya Dubai iunde kampuni ya Tanzania ya kufanya nayo kazi. Zitto alisema kampuni hiyo ndiyo watakaohusika kufanya operesheni na imilikiwe na Tanzania na Dubai (DP World) nusu kwa nusu.

Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Tanzania Bara, Dorothy Semu, alisema ni wakati wa kuhakikisha watu waliotumikia Taifa wanapata kifuta jasho chenye ahueni badala ya kikokotoo kipya kinachotumika sasa. Alikitaja kina maumivu kwa wastaafu.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha KINGOLWIRA**
**Mkoa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. /2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**AMINA AHAMAD RAMADHANI wa KILOKA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA SAKINA ABDALLAH DENGEA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 13 Mwezi 06 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

* Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia *Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 31 mwezi 05 mwaka 2023

MOROGORO

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **PHILEMON REVELIAN KASEIJA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya Fuso lenye namba za usajili **T642 DKM.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/197304/2023.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye.

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **OMARI Y. NKENDA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari lenye namba za usajili **T350 CPR.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/KAR/RB/128066/2023.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye.

---

## TANZANIA COMMISSION FOR UNIVERSITIES

## REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST

**Country:** TANZANIA
**Name of Project:** Higher Education for Economic Transformation (HEET)
**Credit No:** IDA- 68870
**Project ID No:** P-166415
**Assignment Title:** Provision of Consultancy Services for Design Review and Construction Supervision of TCU Office Building on Plot No. 56/4 Block B At Kisasa Centre – Dodoma City
**Reference No.:** PA/073/WB-HEET-P-166415/350606/2022-23/CS/02

1. The Government of the United Republic of Tanzania through the Ministry of Education, Science and Technology (MoEST) has received financing from the World Bank to meet the costs for implementation of the Higher Education for Economic Transformation (HEET) Project and intends to apply part of the proceeds of this fund to cover eligible payments under the contract for Provision of Consultancy Services.

2. The consulting services ("the Services") include carrying out Design Review and Construction Supervision of TCU Office Building. The total duration for the entire assignment shall be twenty nine (29) calendar months where by two (02) month for review design, fifteen (15) months for construction supervision and twelve (12) months for defect liability period. The estimated level of effort is 47.9 Staff-Months.

3. The detailed Terms of Reference (ToR) for the assignment are available in the following website "**www.tcu.go.tz** or can be obtained at the address given below.

4. The **Tanzania Commission for Universities** now invites eligible consulting firms ("Consultants") to indicate their interest in providing the Services. Interested Consultants should provide information demonstrating that they have the required qualifications and relevant experience to perform the Services. The shortlisting criteria are:

**A. Core business and 10 years in business**

**B. Relevant similar experience which should specifically include the following;**

i. The firms should have at least ten (10) years' experience in the building industry, and must have demonstrated capabilities of undertaking works of similar nature, value and volume. Supporting documents of at least three (3) projects of similar nature executed by the firm within the previous ten (10) years (2012 – 2022) is vital-Information to be provided should include name of assignments, names and full contact addresses of the Clients, contract value (in equivalent US dollars) and period (dates) of execution of assignments.

ii. Demonstration of experience of work in similar conditions.

**C. Technical and Managerial Capability of the Firm**
The Consultant must provide the structure of the organization, general qualifications and number of Key staff. (Do not provide CV of the Key staff. Key Experts will not be evaluated at the shortlisting stage).

5. Attention of interested Consultants is drawn to Section III, paragraphs, 3.14, 3.16, and 3.17 of the World Bank's "Procurement Regulations for IPF Borrowers" of November 2020 ("Procurement Regulations"), setting forth the World Bank's policy on conflict of interest.

6. Consultants may associate with other firms to enhance their qualifications, but should indicate clearly whether the association is in the form of a joint venture and/or a sub-consultancy. In the case of a joint venture, all the partners in the Joint Venture (JV) shall be jointly and severally liable for the entire contract, if selected. Therefore, each member of JV shall independently meet the requirements of the evaluation criteria. The experience, technical & managerial capability of the Sub-Consultant shall not be evaluated to enhance the qualification of the Lead Firm or JV.

7. A Consultant will be selected in accordance with the **Consultant's Qualification Selection (CQS)** method set out in set out in the Procurement Regulations.

8. Further information can be obtained at the address below during office hours 08:00 – 15:30 Hours East African Time on Monday to Friday inclusive except on public holidays.

9. Expressions of interest should be submitted online through Tanzania National Electronic Procurement Systems (TANePS) (www.taneps.go.tz) on or before 26th June, 2023 at 1000 Hour's East Africa Time. The Client shall not be held liable for any delays due to system failure beyond its control. Even though the system will attempt to notify the Consultants of any updates, the Client shall not be liable for any information not received by the Consultants. It is the Consultants' responsibility to verify the website for the latest information related to this selection process. Expression of Interests will be opened promptly through TANePS.

**EXECUTIVE SECRETARY**
**TANZANIA COMMISSION FOR UNIVERSITIES**
**P.O. BOX 6562**
**DAR ES SALAAM**

**RIPOTI YA UCHUNGUZI**

## MKASA ASKARI-PORI KUDHURU MBARALI...

# Hofu vijijini, wenyeji waibua yasiyotajwa

**Na Halfani Chusi, aliyekuwa** MBARALI

KATIKA Mkutano wa Bunge la Bajeti unaoendelea jijini Dodoma, siku ya Alhamisi tarehe 11, mwezi uliopita, Mbunge wa Mbarali, Francis Mtega (CCM), aliibua hoja ya wapigakura wake kuteswa na kuunguzwa kwa mapanga ya moto wakiwa uchi.

Watesaji ni askari-pori wanaosimamiwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura ya 282; na lenyewe kusimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Ni madai yaliyoambatanishwa na mengine ya miezi miwili iliyopita, watuhumiwa hao wa utesaji, walipohusishwa na tuhuma za kutaifisha ng'ombe 170 wa wakazi jirani katika mazingira tata na yasiyo ya haki.

Ni hoja iliyomuumiza kichwa Mtendaji Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, naye akachukua uamuzi wa papo kwa hapo, akiagiza timu ya mawaziri watatu, akiwamo wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, waanze safari siku hiyo kwenda eneo la tukio kupata ukweli, kisha warudi kwake siku ya pili na mrejesho.

Ikibaki mada moto, yenye hoja zinazokinzana kati ya walalamikaji wakiongozwa na mbunge na upande wa pili wa serikali, Nipashe wiki mbili zilizopita, asubuhi jua likiashiria mawio, ilifika kijijini Mwanavala wilayani Mbarali kuliko na tukio na kuweka kambi kwa muda wa wiki moja. Ni umbali wa kilomita 20 kutoka mji mdogo wa Igawa, barabara kuu kuelekea Mbeya.

Katika hali isiyo ya kawaida, gari lilipofika kijijini hapo, likaonekana kuzua hofu, wenyeji jamii ya wafugaji walitimua mbio zinazoashiria kuogopa, hadi pale mwandishi alipofanikiwa kumshawishi kijana mmojawapo mwenye ujasiri, ndipo wakaafikiana hata akawa wakala wa kuwatuliza wenzake wasiwe na hofu, kila gari lilipowafikia wenyeji, yeye akiwa ndani akiwatamkia "...msiwe na wasiwasi wala msikimbie, hawa siyo TANAPA..."

Baada ya kumdadisi mwenyeji huyo (jina tunalo), akaanika undani wa taf-





Sehemu ya madhila waliyotendwa wakazi wa Mbarali na askari wa TANAPA hivi karibuni. **PICHA ZOTE: HALFANI CHUSI**

rani zilizotokea mahali hapo, madhara ya mwili, vifo na kupoteza mali, hata kuchangia wakazi wake kubaki na maisha ya hofu.

Udadisi wa Nipashe kupata ukweli, ukaifikisha nyumbani kwa Golyama Mbala (33), anayedaiwa kudhuriwa. Hakuwapo na alipoitwa, ghafla haiba yake ikatawaliwa na hofu, hadi alipothibitishiwa na mwenzake kwa lugha yao 'wow iloo! Kanyodi nale metii', akimaanisha 'njoo bwana hakuna tatizo'.

Ni aina ya mazungumzo ndani ya nyumba, wanafamilia wote walikuwa wamezunguka kufuatilia kinachoendelea kwa 'watu wema' na waliporidhika nao, ghafla nafsi zikahamia katika bashasha.

Mbala anasimulia siku hiyo majira ya saa saba mchana akiwa machungani, ghafla aliona chopa ikishuka kumfuata aliko na kadri ilivyomsogelea, ng'ombe wake wapatao 130 wakaanza kukimbia kueleka upande uliko mpaka wa Hifadhi ya Taifa Ruaha.

Analalamika ni tukio lililomshtua, hata akachukua uamuzi wa haraka kukimbilia mbele kujaribu kuwadhibiti ng'ombe warejee kijijini, lakini akazidiwa, kwani staili ya ujio wa chopa hiyo ilikuwa inawaswaga kuelekea hifadhini.

Anasema kadri ushindani ulivyopamba moto, chopa ikashuka zaidi na ghafla askari waliokuwamo ndani wakaruka kwa stadi za kijeshi na kuanza kumvamia kwa kipigo.

Anasimulia wakati ndege hiyo ilikuwa imepaki pembeni, walimvua nguo kwa nguvu, wakamuunguza kwa mapanga waliyoyatoa katika eneo la injini ya ndege yakiwa ya moto sana, kwenye maeneo tofauti ya mwili; kichwani, mgongoni, makalio, mapajani, kifuani na mabegani.

Anasimulia ni mateso waliyoendelea nayo, huku mavazi waliyomvua wakawa wanayachoma moto, walioutumia kupasha mapanga moto ili kuendeleza kumuunguza, wakati wote huo mikono yake ilikuwa imefungwa kwa pingu, imeshikamanishwa kulizunguka gogo na wakati



huo mbwa watatu alioambatana nao walipigwa risasi na kuuawa papo hapo.

"Kuna mmoja alisema 'maliza kabisa huyo, atatusumbua mmiminie risasi', lakini akatokea yule aliyekuwa anaendesha ndege, mwanamke mzungu akasema 'hapana msimuue, tumtese mpaka akome!'" anasimulia huku akionyesha majeraha.

Simulizi hiyo ya mambo yenye kumbukumbu za mateso, zilimuingiza ghafla katika huzuni... anaendelea: "Baada ya hapo wakaniacha nikiwa katika hali mbaya, mwili mzima unauma, sijiwezi, nikawa nimelala, mpaka alipotokea mtu nikamwagiza nyumbani, ndipo wakaja kunifuata na 'powertiller' (pikipiki ya matairi matatu)."

Anasema kunusurika ng'ombe wake ni pale walipogeuza mwelekeo wakati wa purukushani na kufuata njia ya kuelekea nyumbani zizini.

Ni simulizi inayoshabihiana na ile Nipashe ikaanikiwa tena na mwenyeji aliyempokea mwandishi kijijini hapo, mara hii ni umbali wa kilomita kadhaa, mkasa huo ukiwahusu kinamama watatu na mwanamume waliovuliwa nguo, wakateswa wakiwa hawana nguo, watuhumiwa ni walewale - askari-pori, ikielezwa kuwa baada ya kumwacha mchungaji wa kwanza taabani, walishuka na chopa yao kwa staili ileile katika eneo tofauti wakiendesha mateso mengine.

Huku akionyesha majeraha yao, Anna Saturu, anasimulia mkasa wao kwa niaba ya wanawake, wenzie wawili Rehema Saturu (21) na Doris Saturu (21), akisema: "Walitukuta tunachuma mboga, wakatuuliza 'kwanini mnachuma mboga hifadhini?' Tukawaambia huwa tunakuja kuchuma hapa, wakasema 'hili ni eneo la hifadhi', wakaanza kutupiga huku wanatuvua nguo kwa nguvu...

"Wakawa wanatupiga na mapanga yenye moto mimi na wenzangu wawili, baadaye walipotosheka, akashuka rubani, alikuwa mzungu, akasema 'waache', ndipo wakatuacha. Lakini tulikuwa katika hali mbaya, mwili mzima ulikuwa unauma na tulichanganywa na mwanamume, wote tulikuwa uchi."

Ni ukatili unapokinzana na maelekezo ya Ibara ya 15(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inayoelekeza kuhifadhi haki ya mtu kuwa huru na kuishi kwa uhuru, ikipiga marufuku mtu yeyote kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini au kunyang'anywa uhuru wake.

Nipashe ikahamia kupata maelezo ya mwanamume huyo, Mage Nharamila (33), akawa na ufafanuzi wenye mengi ya mateso yanayofanana na ya mwenzake katika mkasa wa awali. Hata hivyo anayo ya ziada, anayoyasimulia huku akitokwa machozi:

"Walinifunga mikono kwenye gogo na pingu yao, kisha wakanivua nguo zote, wakawasha moto mbele yangu, wakaweka mapanga, yalipopata moto, wakaanza kunichoma nayo, huku wananigonga na virungu kwenye kiwiko cha mkono, magotini na kwenye unyayo.

"Waliniumiza sana! Nilishindwa hadi kutembea. Hata hapa nilipo, siwezi kufanya shughuli yoyote, mambo yangu bado magumu sana, mwili wangu una maumivu makali. Kitu kilichoniumiza zaidi ni kuwekwa uchi mbele ya wanawake ambao ni kama ndugu zangu na tulikuwa tunaheshimiana sana!"

Udadisi wa Nipashe ukahamia kwenye mkasa mwingine wa kifo cha kijana Urande Kungila. Kilitokea mwaka 2021. Baba yake mzazi, Dotto Shigela, anadai askari wa hifadhi ndio wahusika wakuu.

Anaeleza: "Nililetewa taarifa na wasamaria wema kuwa mwanangu amezidiwa, ndipo tukakurupuka kwenda huko, tukamkuta damu zinavuja, amepigwa risasi mgongoni na askari wa TANAPA.

"Baada ya hapo tukampeleka hospitalini, lakini haikuwa riziki. Kilichoniumiza zaidi, katika maelezo ya kifo cha mwanangu walitaka kulazimisha aonekane risasi imepigwa kuanzia kifuani kuja mgongoni, mradi tu ionekane alikuwa anapambana na askari."

Nipashe ikafika mezani kwa viongozi: Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mapinduzi, Yasaire Kimosa; Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwanavala, Chesco Kapunga; na Ofisa Mtendaji wa Kata Imalilo Songwe, Angelina Mtweve, wote kwa nyakati tofauti wakathibitisha kuwapo matukio hayo, hoja ambayo pia iliungwa mkono na uongozi wa wilaya.

***Fuatilia kesho majibu ya serikali na mzizi wa mgogoro .**




Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani wa NSSF, Godfrey Ngonyani (kulia), kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba (hayupo pichani), akimkabidhi Rais wa Chama cha Majaji na Mahakimu Tanzania (JMAT), Jaji John Kahyoza, zawadi kwa niaba ya Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mustapher Siyani (hayupo pichani) baada ya Jaji Kiongozi kufungua semina ya siku mbili kwa majaji na mahakimu wa Kanda ya Ziwa, Tabora, Manyara na Kigoma kwa njia ya mtandao kupitia e-Mikutano. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ucheleweshaji michango mifuko ya hifadhi wadhorotesha haki

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

CHAMA cha Majaji na Mahakimu Tanzania (JMAT), kimesema ucheleweshaji wa michango ya wanachama unaofanywa na baadhi ya waajiri katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inadhorotesha haki za wanaostahili kupata mafao yao kwa wakati.

Hayo yamesemwa na rais wa JMAT, Jaji John Kahyoza ambaye ni Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Manyara, wakati wa semina ya siku mbili iliyofanyika mwishoni mwa wiki, jijini hapa.

Semina hiyo iliandaliwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kwa ajili ya majadiliano ya pamoja baina ya Mfuko na Majaji na Mahakimu wa Kanda ya Ziwa, Tabora, Manyara na Kigoma, iliyokuwa na kaulimbiu 'Utoaji haki kwa wakati kwa ustawi wa hifadhi ya jamii'.

"Kupitia semina hii tumejifunza kuwa ucheleweshaji wa michango katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii unadhorotesha uchumi na haki za wanaostahiki kupata mafao," alisema Jaji Kahyoza.

Kahyoza alisema katika semina hiyo waligusia maeneo mbalimbali ya uendeshaji wa mifuko na changamoto unazokabiliana nazo na namna nzuri ya kuzitatua na kuwa wanachama wa JMAT wamefahamu mafao yanayotolewa na NSSF pamoja na mchango wa Mahakama katika kuhakikisha ustawi wa hifadhi ya jamii unazidi kuimarika.

Kaimu Mkurugenzi wa Sheria wa NSSF, Geoffrey Sikira, alisema mfuko una mashauri 350 katika mahakama mbalimbali yakiwamo yanayohusiana na madai ya michango yaliyoshindwa kuwasilishwa na waajiri na kusababisha wanachama kushindwa kupata haki zao kwa wakati.

# Mtaalamu: Uhifadhi unaondoa hewa ukaa kwa asilimia 37

**Na Salome Kitomari**

MAENEO yaliyohifadhiwa nchini yananyonya asilimia 37 ya hewa ukaa iliyopo angani, jambo linalohitaji jitihada zaidi katika kukabili mabadiliko ya tabianchi.

Hayo yameelezwa hivi karibuni na wataalamu wa uhifadhi wa shirika lisilo la kiserikali la RTI ambalo ni Mshirika Mtekelezaji wa USAID wakitekeleza mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili Activity.

Meneja Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi, RTI, Mshiriki Mtekelezaji wa Mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili Actibity, Dk. Elikana Kalumanga, alisema maeneo yaliyohifadhiwa ni nyenzo muhimu katika kupambana na uharibifu wa bionuwai.

Alisema licha ya Tanzania kutoa mchango mkubwa kwenye kukabili mabadiliko ya tabianchi, bado mchango halisi wa bionuwai haujaonekana vyema kwenye pato la taifa."Kwa sasa mchango wake ni asilimia 3.5, lakini ukifuatilia kwa kina bado kuna mchango kubwa zaidi, mfano maji tunayotumia na kupatikana wake na kiasi tunacholipa ndiyo thamani halisi?" Alihoji.

Alisema binadamu hana budi kutunza vyema mazingira kutokana na umuhimu wake kwenye afya yake, huku akitoa mfano wa nchi za Canada na Marekani ambazo zinatafuta nyuki kwa ajili ya uchavushaji mazao kutokana na kutopatikana.

"Hivi karibuni kulikuwa na kesi ya mkulima huko Canada ambaye alinyunyuzia dawa kwenye mazao yake bila kujua kwamba wenzake walileta nyuki kwa gharama kubwa kwa ajili ya uchavushaji, na sasa anadai mabilioni ya fedha. Hii inaonyesha thamani ya wadudu kwenye mazao," alisema.

Dk. Kalumanga alisema kuna watu wameharibu maeneo yao kiasi cha kukosekana wadudu muhimu na kwamba uhifadhi pekee ndiyo utakaorudisha uoto wa asili kwa kuwa binadamu anategemea mazingira na mazingira yanamtegemea binadamu.

Mtaalamu huyo alishauri hatua za kuchukua ni pamoja na kuwa na mpango wa kuhifadhi mazingira na kufanya shughuli za kibinadamu kwa uangalifu mkubwa kwa kuwa yanategemewa katika kupata hewa safi, uchumi, kilimo, teknolojia na kijamii.

Meneja Ufuatiliaji na Tathmini, RTI, Mshiriki Mtekelezaji wa USAID inayotekeleza Mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili, John Noronha, alisema ni muhimu kila mmoja kuwajibika nje ya eneo lake la utawala na kuwa na mikakati ya muda mrefu ya kutenga rasilimali na kwamba kukiwa na mkakati endelevu wa kuokoa mazingira.

Aidha, alisema ni muhimu wananchi wakaelimishwa muhimu wa kutunza mazingira ikiwamo biashara ya hewa ukaa huku akitoa mfano eneo la Nantakara, West Kilimanjaro lenye vijiji vinane vyenye ukubwa wa ekari 216,00 vinavyokaliwa na watu 1,700 na kuata Dola za Kimarekani 700,000 kutokana na kuhifadhi miti milioni 1.25.

Kwa mujibu wa Noronha, kwenye uhifadhi kuna fursa nyingi ikiwa jamii itafundishwa kuziona na kuzitumia, na kwamba ikiwa hivyo uharibifu wa mazingira hautakuwapo.

Mkuu wa Sehemu ya Utangazaji Utalii Ikolojia wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Anna Lauwo, alisema kuna utaratibu wa kuvuna misitu maeneo yaliyohifadhiwa ili kuwa na uendelevu na wamekuwa wakielimisha jamii kuhusu kulinda maliasili kwa faida ya maisha ya sasa na vizazi vijavyo.

# Puma Energy kutoa gawio la bil. 12/- kwa wanahisa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Puma Energy itatoa gawio la Sh. bilioni 12.2 kwa wanahisa wake, ikiwamo serikali kwa mwaka 2022. Katika kikao chake cha wanahisa kilichofanyika wiki iliyopita, Mwenyekiti wa Bodi ya Puma Energy Tanzania, Dk. Selemani Majige na Fatma Abdallah, Meneja Mkuu, walikabidhi hundi za mfano kwa wanahisa wa Puma Energy Tanzania, ambao ni Msajili wa Hazina na Puma Investments Limited, wawakilishi wa wanahisa wakiwa ni Nehemia Mchechu na Fadi Mitri, walipokea gawio la kipindi cha mwaka 2022.

Akizungumza katika hafla hiyo, Abdalla, alithibitisha kuwa Puma Energy Tanzania iliripoti faida halisi ya Sh. bilioni 24.4 (USD 10.32 milioni) kwa mwaka ulioishia Desemba 2022 na gawio lililolipwa kwa wanahisani Sh. bilion 12.21 (Dola za Kimarekani milioni 5.15) ambayo ni asilimia 50 ya faida halisi ya kampuni kwa mujibu wa sera ya gawio. Mgawo huo ulitangazwa kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa wanahisa wa kampuni uliofanyika Mei 10, mwaka huu. Kwa kuzingatia sera ya gawio, Sh. bilioni 7.3, ikiwa ni asilimia 30 ya faida halisi ya kampuni kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2022 zitatengwa kwa ajili ya uwekezaji wa kampuni na Sh. bilioni 4.88 (asilimia 20) ya faida halisi ya kampuni zitahesabiwa kama mapato ya kampuni.

Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu, aliipongeza serikali kwa ushirikiano ulioanzishwa na Kampuni ya Puma Energy, akionyesha msimamo wa kuunga mkono serikali ya awamu ya sita katika kudumisha sera ya ushirikiano na sekta binafsi.

Mchechu alisisitiza kuwa ushirikiano huo, kama serikali inavyoshirikiana na Puma Energy, unanufaisha pande zote, serikali na washirika wake wa sekta binafsi.

Alitoa rai kwa bodi na menejimenti ya Puma Energy Tanzania, kuendelea kuwa wabunifu wa huduma mbalimbali na alisisitiza kuona umuhimu wa kupanua shughuli za Puma Energy nje ya Mkoa wa Dar es Salaam, akibainisha kuzidi kuwapo fursa kutokana na ukuaji wa miji mbalimbali sasa kwa kasi kubwa.

Mchechu aliipongeza Kampuni ya Puma Energy kwa utendaji kazi wake uliotukuka hadi sasa na jitihada za kampuni hiyo kuwekeza katika nishati mbadala hususani zilizoanzishwa karibuni kama huduma za gesi ya LPG, matumizi ya nishati ya jua na CNG.

Fadi Mitri, Mtendaji Mkuu wa Puma Energy, Kanda ya Afrika, alisema: "Hundi za gawio zilizotolewa leo zinadhihirisha mchango chanya wa ushirikiano kati ya Puma Energy na Serikali ya Tanzania katika kusaidia ukuaji wa uchumi. Puma Energy ina jukumu muhimu la kupeleka huduma za nishati sehemu mbalimbali nchini sambamba na kusaidia jamii.

"Kwa kutumia mnyororo wetu wa kimataifa wa usambazaji, tumeweza kufanikisha usambazaji wa mafuta yetu yenye viwango vya juu vya ubora wakati wa changamoto ya hali ngumu ya soko la kimataifa. Suala lingine muhimu zaidi, faida iliyopatikana tumeigawanya sawa na Watanzania kupitia malipo haya ya gawio kwa serikali."

Meneja Mkuu wa Kampuni ya Puma Energy Tanzania Limited, Fatma Abdallah, aliwashukuru wanahisa wa kampuni hiyo na Bodi ya Wakurugenzi kwa msaada na miongozo yao isiyoyumba na juhudi zao za pamoja kwa ushirikiano na wafanyakazi zimewezesha kampuni kupata mafanikio husussan katika kipindi kigumu cha kukabiliana na changamoto zilizotokana na janga la ugonjwa wa Covid-19.

Fatma amebainisha kuwa Puma Energy Tanzania inashirikiana kikamilifu na serikali katika kukabiliana na changamoto mbalimbali za kibiashara, ikiwamo nakisi ya Dola za Kimarekani.

Alisisitiza kuwa anaamini kuwa changamoto hizo zikipatiwa ufumbuzi ipasavyo, utendaji wa Puma Energy Tanzania utazidi kukua kibiashara. Kampuni bado ina dhamira ya kuendelea kutoa huduma bora na za kisasa kwa wateja wake, huku ikiendelea kutekeleza dira yake ya kuwezesha jamii katika maeneo inakofanyia biashara zake.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Hili la tuzo kamati ilifanyie kazi kuondoa mvutano

**MSIMU** wa Ligi Kuu 2023/2024 ulimalizika rasmi Ijumaa iliyopita kwa Yanga kukabidhiwa kombe la ubingwa wakiwa wamefanya hivyo kwa miaka miwili mfululizo.

Yanga walistahili ubingwa huo kwa namna walivyojiandaa kabla ya kuanza kwa ligi na namna walivyopambana katika michezo yao yote. Kumalizika kwa ligi msimu huu ni mwanzo wa maandalizi ya msimu ujao wa Ligi Kuu, msimu wa 2023/2024.

Maandalizi haya si kwa klabu, wachezaji peke yake, lakini kwa Shirikisho na wadau wake wengine kuhakikisha msimu ujao unakuwa bora zaidi ya msimu huu.

Pamoja na msimu huu uliomalizika kwenda vizuri kukiwa na ushindani mkubwa ndani na nje ya uwanja, bado kulikuwa na kasoro ndogo ambazo tunaamini wahusika watazifanyia kazi ili kuiboresha ligi yetu ambayo imetajwa kuwa miongoni mwa ligi bora Afrika.

Hakuna ubishi msimu ulikuwa na ushindani mkubwa, kuanzia ndani ya uwanja mpaka nje ya uwanja, kulikuwa na ushindani wa mchezaji mmoja mmoja na timu kwa ujumla wake, hii yote ilileta burudani na msisimko kwa mashabiki.

Kila kitu kilikuwa wazi kuelekea mwishoni mwa msimu wa ligi, kila mechi zilipokuwa zinachezwa ilikuwa inaonekana wazi nani anaenda kujiweka kwenye mazingira mazuri na nani anachimbia shimo la kushuka daraja, mwisho wa siku kila mmoja kavuna alichokipanda.

Eneo kubwa ambalo limeleta ubishani na mvutano baada ya mchezo wa mwisho wa ligi yetu ni sehemu ya tuzo ya mfungaji bora wa ligi. Awali ilionekana kama hakutakuwa na mvutano wowote kwa sababu kuu mbili za kuamua nani atakuwa mfungaji bora wa ligi yetu kwa msimu wa 2023/2024.

Kwanza kulikuwa na utofauti mkubwa wa wafungaji, Mayele alionekana wazi anaenda kutwaa tuzo hii kutokana na kasi yake ya ufungaji na idadi kubwa ya magoli aliyokuwa nayo ukilinganisha na anayemfuata ambaye alipishana naye kwa mabao sita.

Tatizo limekuja pale wachezaji wawili walipofungana kwa idadi ya magoli, Mayele na Ntibazonkiza ambao wote walifikisha idadi ya mabao 17, ushindani ukaanzia hapo.

Mabishano yaliyopo ni wazi yanatokana na kutokuwapo na kanuni za wazi kuelekeza pale wafungaji wanapolingana kwa idadi ya mabao mengi nani anapaswa kutwaa tuzo hiyo.

Kutokuwapo kwa kanuni hizo za wazi ndizo zimeleta ubishani kwa mshabiki wa Simba na Yanga kila mmoja akivutia kwake kutaka kuona mchezaji wake anachukua tuzo bila kuangalia kanuni.Kamati ya tuzo iliyopo inapaswa kuchukulia hili kama changamoto inayokwenda kutatuliwa, ni vyema kanuni za kuamua mfungaji bora ni nani pale wachezaji wawili au na zaidi wanapofungana kwa idadi ya mabao mengi.


Kama kanuni zinakuwa wazi tangu mwanzo, mara filimbi ya kumaliza mchezo wa mwisho inapopigwa moja kwa moja kwa kutumia kanuni mfungaji bora anapatikana hata kama kutakuwa na idadi ya wachezaji zaidi ya wawili watakalingana kwa ufungaji.

Kinachotokea sasa ni mvutano wa 'mimi nastahili' kwa sababu hakuna kanuni za wazi, ingawa Bodi ya Ligi imeweka wazi kamati itaamua nani anastahili kuwa mfungaji bora, haikupaswa kusubiri kamati kwa sababu tuzo hiii ni ya wazi.

Tunashauri mwanzoni tu mwa msimu ujao kamati hii iweke wazi kanuni zitakazoamua nani atakuwa mfungaji bora pale wachezaji wawili au na zaidi wanalingana kwa idadi ya mabao mengi, hii itaondoa mvutano huu uliopo ambao sasa watu wanaanza kufikiria kuna 'figisu' zinaenda kufanyika katika kuamua nani atangazwe kuwa mfungaji bora.

Tunatarajia kuona msimu ujao kanuni hizi za tuzo zitawekwa wazi hasa kwenye tuzo hii ya mfungaji bora na vipengele vyake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

### Muungwana Lazima Nilonge

## Kanuni za Ligi Kuu hazitakiwi kufichwa kama 'mihadarati'

**HADI** leo hii hakuna yeyote anayefahamu ni nani atakayechukua kiatu cha dhahabu kati ya straika wa Yanga, Fiston Mayele na Saido Ntobazonkiza wa Simba.

Wote wamepachika mabao 17 mpaka msimu wa 2022/23 umemalizika, hata waandishi wa habari walipouliza ni vigezo gani vinatumika kwa ajili ya kumpata mshindi mmoja, Ofisa Habari wa Bodi ya Ligi, Karim Boimanda, akasema kazi yote imeachwa kwa Kamati ya Tuzo ambayo ndiyo itaamua ni nani mshindi.

Inawezekana mmoja kati yao akatwaa mshindi wa ufungaji bora msimu huu, au wote wawili wakakabidhiwa kiatu kama ilivyokuwa msimu wa 2016/17 wakati aliyekuwa Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF) wakati huo, Jamal Malinzi, alipoamua wachezaji Simon Msuva wakati huo akiichezea Yanga na Abdurahman Mussa, wote wapewe zawadi ya ufungaji bora walipomaliza wakiwa na mabao 14 kila mmoja.

Inavyoonekana hata wakati huo hakukuwa na kanuni yoyote inayoonyesha ni nani atakuwa na haki ya kukipata kama wakifungana.

Rais Malinzi kwa mamlaka yake akaamua kuwapa wote wawili na ndiyo maana hakusubiri kamati, akaamua kisiasa.

Ni misimu mingi imepita baada ya tukio hilo, la kushangaza ni kwamba bado Bodi ya Ligi na kamati zake haijajifunza kutokana na hilo.

Mpaka sasa hakuna yeyote anayefahamu kama kanuni ipi inatumika kama wachezaji wawili wakifungana mabao pia haijulikani kama kweli kanuni hizo zipo au hakuna.

Ndiyo maana kumekuwa na ubishani mkubwa mitaani, vijiweni na sehemu mbalimbali ambazo wanamichezo wanakutana juu ya nani anatakiwa kuwa mfungaji bora kati ya Mayele na Saido.

Cha kushangaza hata wanahabari, wakiwamo wachambuzi nao wanabishana juu ya nani anatakiwa kupata kiatu cha dhahabu. Hili suala linachekesha na kuhuzunisha kwa wakati mmoja.

Baadhi wanatumia kanuni za misimu iliyopita ili kujenga hoja kuwa mchezaji fulani anatakiwa awe mfungaji bora, wengine wapo kishabiki zaidi.

Hii yote haikupaswa kuwa hivi kama kweli kungekuwa na kanuni tangu kuanza kwa Ligi Kuu msimu huu, au hata kama ipo kanuni zilitakiwa kuwa wazi na si kufichwa kama mihadarati.

Kanuni haziwezi kuwa zinajulikana na wanakamati tu ya tuzo, labla tu watuambie msimu huu hawakuwa na aina hiyo ya kanuni.

Hata hivyo bado itashangaza kwa sababu matukio haya ya kufungana hujitokeza sana katika michuano mbalimbali, Ligi Kuu au michuano mingine duniani, ikiwamo hata Kombe la Dunia.

Kwa sababu kila msimu kunakuwa na kanuni yake, basi ilipaswa kujulikana wazi kwamba wachezaji wakilingana mabao, basi atakayekuwa na usaidizi mwingi wa mabao 'assist' ndiye awe mshindi au aliyecheza dakika chache kuliko mwenzake apewe tuzo, au asiye na mabao ya penalti au machache kuliko mwenzake.

Haya yangekuwapo hata hizi kelele tusingezisikia kwa sababu kila mmoja angejielekeza kwenye kanuni inasemaje tu basi.

Vyovyote itakavyokuwa, lakini sasa hili liwe funzo kwa Bodi ya Ligi na kamati zake wanapotengeneza kanuni wasikae nazo kimya, badala yake wawe wanaziweka hadharani kwa kutumia njia mbalimbali, ikiwamo kuchapisha kwenye mitandao yao ya kijamii ili kila mwanamichezo azisome.

Hata wanahabari wao wanatakiwa mapema tu waanze kuziuliza na kuzifuatilia kanuni na si kusubiri mpaka kutokee utata kama huu, kwani inaonekana nao wanakuwa kama wapo upande fulani, au habari zao zinaegemea zaidi linapokuja suala la Simba na Yanga.

Msimu ujao kanuni zinatakiwa ziwekwe wazi, kwenye ufungaji bora iwapo wachezaji wakilingana kwa mabao, 'clean sheets' kwa makipa na vipengele vingi ambavyo wanaona vinaweza kuleta utata mbele ya safari.

# RCC yamaliza mvutano eneo ujenzi chuo kikuu

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amesema chuo kikuu cha serikali mkoani mwake kitajengwa makao makuu ya mkoa huo yaliyoko Halmashauri ya Mji wa Njombe.

Alitangaza hayo jana katika kikao cha Kamati ya Ushauri wa Mkoa (RCC) kilichokuwa na ajenda moja ya kujadili mahali ambapo chuo hicho kitajengwa baada ya kuwapo mvutano kuhusu eneo la kujenga chuo kikuu hicho.

Mtaka alisema kikao cha RCC kimepokea kusudio la serikali la kujenga chuo kikuu katika Mkoa wa Njombe.

Alisema maelekezo ya uongozi wa chama kwa serikali mkoani Njombe ni kuwasilisha maombi Wizara ya Elimu na chuo ambacho kitajenga kampasi yake mkoani hapa kijengwe makao makuu ya Mkoa wa Njombe.

Alisema kama ambavyo Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe alivyoelekeza na kushauri kuwa chuo hicho kikuu kitakuwa cha kwanza kujengwa mkoani hapa, hivyo kijengwe makao makuu ya mkoa ili kukuza na kuchangamsha makao makuu ya mkoa.

"Kwa pamoja kama Mkuu wa Mkoa ninaomba sasa rasmi Katibu Tawala uiweke kwenye maandishi - kikao cha ushauri cha mkoa kimepokea ushauri na maelekezo ya chama kwamba kwanza kinamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa serikali kuonyesha kusudio la kujenga Chuo Kikuu Mkoa wa Njombe.

"Mkoa utapitia maeneo matatu ya Halmashauri ya Mji Njombe na wataalamu waje kujiridhisha eneo litakalojengwa chuo kikuu pindi fedha zitakapopatikana," alisema Mtaka. Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe, Judica Omary, alisema serikali imeonyesha nia ya kutoa fedha kwa ajili ya kujenga chuo kikuu katika Mkoa wa Njombe.


Alisema ofisi ya mkoa imepokea maombi ya ujenzi wa chuo hicho kutoka halmashauri mbili za mkoa huo ambazo Halmashauri za Mji wa Njombe na Makambako.

"Katika Halmashauri ya Mji wa Njombe imejipanga na kupitisha suala hili katika vikao vyake vya kisheria juu ya uhitaji wa kujenga chuo kikuu na maeneo yameshaainishwa na kwa upande wa Makambako nayo imepitisha katika vikao vyake vya kisheria juu ya uhitaji wa kujenga chuo kikuu," alisema Omary.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Njombe, Deo Sanga, alisema kikao hicho kimefanyika kutokana na sintofahamu ya maneno kutoka kwa baadhi ya watu kuwa chuo hicho kinataka kuhamishwa na kupelekwa moja ya halmashauri iliyopo mkoani Njombe, jambo ambalo siyo kweli.

Mbunge wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika, alisema wakati mkoa huo unaomba kujengewa chuo kikuu, mjadala haukuwa sehemu ambayo chuo hicho kitajengwa kwa kuwa ilikuwa inafahamika chuo hicho kitajengwa makao makuu ya mkoa huo kama ilivyo katika maeneo mengine nchini.

"Wakati tunaomba chuo kikuu wengi tulikuwa hatusemi sana kuhusu eneo litakalojengwa chuo hicho kwa kuwa kila mtu alikuwa anajua ni wazi kwamba tukipata nafasi ya kujenga chuo kikuu cha kwanza kitakaa makao makuu ya mkoa," alisema Mwanyika.




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (kushoto) sambamba na Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi, wakionesha mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 100 zilizotolewa na benki hiyo ili kufanikisha mpango wa ufadhili wa masomo ya ufundi stadi kwa vijana 1,000 kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ujulikanao kama 'NBC Wajibika Scholarships'. Hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CRDB yaweka rekodi gawio serikalini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amepokea gawio kubwa zaidi kupata kutolewa na taasisi ya kifedha nchini la Sh. bilioni 45.8 linalotokana na uwekezaji wa serikali ndani ya Benki ya CRDB kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya benki hiyo, Dk. Ally Laay.

Makabidhiano hayo ya hundi kifani yalifanyika katika Makao Makuu ya Benki ya CRDB jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Natu El- Maamry na viongozi mbalimbali wa taasisi na mashirika ya umma yenye hisa ndani ya Benki ya CRDB.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mwigulu aliipongeza benki hiyo kwa kutoa gawio kwa serikali, pia kwa kupata matokeo mazuri ya fedha mwaka 2022 ambayo yameongeza gawio kwa wanahisa ikiwamo serikali.

"Ongezeko hili la gawio ni kiashiria tosha kwa serikali kuwa Benki yetu ya CRDB inazidi kuimarika zaidi kutokana na mikakati madhubuti ya kibiashara iliyojiwekea na jambo linalowapa moyo Watanzania na wawekezaji kuwa benki inatoa huduma bora katika jamii," alisema. Waziri Mwigulu alisema fedha zilizopatikana kupitia gawio hilo zitasaidia utekelezaji wa miradi ambayo serikali imeainisha katika vipaumbele vya bajeti ya mwaka 2023/24.

"Kipekee kabisa niipongeze bodi, menejimenti na wafanyakazi wote wa Benki ya CRDB kwa kazi nzuri mnayoifanya," alisema Dk. Mwigulu.

Aliipongeza Benki ya CRDB kwa kukamilisha mkakati wa muda wa kati wa 2018/2022 kwa mafanikio makubwa ambapo katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, faida ya benki hiyo imekua kwa asilimia 875. "Niwapongeze pia kwa matokeo ya fedha ya robo ya kwanza ya mwaka huu ambapo benki yetu hii imepata faida baada ya kodi ya Sh. bilioni 90, mkiendelea na kasi hii mwakani tunategemea kupata gawio nono zaidi," alisema.

Akifafanua namna serikali inavyoridhishwa na umahiri wa Benki ya CRDB katika kufanya biashara kiushindani, Dk. Mwigulu aliipongeza benki hiyo kwa kupanua wigo wake kwa kuanzisha kampuni tanzu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kampuni tanzu ya CRDB Insurance Co. Ltd na CRDB Bank Foundation ambayo imeonyesha kuwa mstari wa mbele katika kuchochea ujumuishi wa kiuchumi kupitia programu ya IMBEJU. Waziri huyo alizitaka taasisi nyingine kuiga mfano wa Benki ya CRDB katika kuleta faida kwa serikali na wanahisa kutokana na uwekezaji.

Alizitaka taasisi na mashirika yote ambayo serikali ina hisa, kuweka mikakati madhubuti itakayoleta tija, huku akiwataka viongozi ambao taasisi zao zimeendelea kuwa na matokeo mabovu kujitathmini kiutendaji.

Waziri Mwigulu aliihakikishia Benki ya CRDB na wadau wengine wa maendeleo nchini kuwa serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan itaendelea kuimarisha na kuweka mazingira rafiki na endelevu ya kufanya biashara katika sekta ya fedha na sekta nyinginezo ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje. Dk. Mwigulu alisema serikali ina mpango wa kuja na programu kabambe ambayo itasaidia kuboresha sekta binafsi na kupunguza mikopo chechefu nchini.

Pia alisisitiza juu ya weledi wa wafanyakazi wa benki katika utoaji wa mikopo kwa kuhakikisha fedha zinazokopeshwa zinakwenda katika miradi au biashara endelevu.

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Natu, aliipongeza Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya Benki ya CRDB kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kusimamia benki hiyo na kupelekea matokeo mazuri ya kifedha na kukua kwa gawio kwa wanahisa ikiwamo serikali.

Dk. Natu pia aliipongeza Benki Kuu kwa usimamizi mzuri wa sekta hiyo ambayo imechangia katika utendaji mzuri wa taasisi za kifedha na kuwapo huduma bora na nafuu kwa wananchi.

Akikabidhi gawio hilo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya CRDB, Dk. Laay, alisema gawio hilo ni sehemu ya faida ya Sh. bilioni 351.4 baada ya kodi ambayo benki hiyo imeipata katika mwaka 2022.

"Katika Mkutano wa Wanahisa uliofanyika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) mwezi Mei mwaka huu, wanahisa wa Benki ya CRDB walipitisha kwa pamoja gawio la Sh. 45 kwa hisa ikiwa ni ongezeko la asilimia 25 na hivyo kufanya jumla ya gawio la mwaka huu kufikia Sh. bilioni 117.5," alisema Dk. Laay.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema kukua kwa thamani ya uwekezaji wa wanahisa wa benki hiyo kutokana na mafanikio ambayo benki hiyo imeyapata katika utekelezaji wa mkakati wake wa biashara wa muda wa kati wa mwaka 2018 - 2022.

Nsekela alisema katika kipindi hicho, Benki ya CRDB imepata mafanikio makubwa ya kiutendaji yaliyopelekea benki hiyo kuwa na mchango mkubwa katika kusaidia jitihada za maendeleo nchini.

Nsekela alibainisha kuwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, benki hiyo imelipa jumla ya kodi ya Sh. trilioni 1.1 kwa serikali. "Katika kipindi cha miaka mitano pia tumeongeza ajira zaidi ya 600 nchini, tukitumia zaidi ya Sh. trilioni 1.3 kulipa mishahara na marupurupu, tumefanya kazi na wazabuni zaidi ya 1,000 na kulipa zaidi Sh. bilioni 625," alisema Nsekela huku akibainisha benki hiyo imetumia zaidi ya Sh. bilioni 14 katika miradi ya kijamii kupitia sera yake ya uwekezaji kwa jamii.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**





Mkuu wa Wilaya ya Ngara, Kanali Mathias Kahabi (aliyevaa kofia), akipokea baadhi ya vifaa vya usafi vilivyotolewa na Kampuni ya Tembo Nickel na kuwasilishwa na Ofisa Mazingira Mwandamizi wa kampuni hiyo, Digna Isdory. Tembo Nickel ilitoa vifaa hivyo kwa Wilaya ya Ngara, ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Wiki ya Mazingira Duniani, wengine pichani ni wafanyakazi wa kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki yajitosa mkakati wa kumtua mama kuni kichwani

**Na Halfan Chusi**

BENKI ya Exim Tanzania imethibitisha nia yake ya kuunga mkono jitihada za serikali za kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia hususani kwa wanawake kupitia adhma ya Rais Samia Suluhu inayolenga kumtua mama kuni kichwani.

Hatua ya benki hiyo inakuja huku tayari serikali kupitia Wizara ya Nishati ikiwa imetangaza kutenga zaidi ya Sh. bilioni 30 kwa ajili ya kusambaza, kununua vifaa vya nishati mbadala ambavyo itavisambaza nchi nzima ili kutimiza azma hiyo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Dhamira ya benki hiyo imebainishwa na Mkuu wa Kanda wa Benki ya Exim Tanzania, Elizabeth Mayengo, wakati akizungumza katika mafunzo ya namna ya kutumia nishati mbadala kwa mama lishe na vijana yaliyoandaliwa na Mtandao wa Uwezeshaji Wanawake Tanzania (TAWEN) mwishoni wa wiki jijini Dar es Salaam. Mafunzo hayo yalizinduliwa na Waziri wa Nishati, January Makamba.

Akifungua mafunzo hayo, Waziri January, alisema serikali imedhamiria kweli kuwasaidia wanawake nchini pamoja na makundi mengine kuondokana na matumizi ya nishati zisizo salama ikiwamo matumizi ya kuni na mkaa kwa kuwa mbali na kuongeza athari za kimazingira, nishati hizo zimekuwa zikiathiri afya ya watumiaji.

"Kuonyesha kwamba tumedhamiria kwenye hili kupitia bajeti hii mpya tumetenga fedha zaidi ya Sh. bilioni 30 kwa ajili ya kusambaza, kununua vifaa vya nishati mbadala ambavyo vitasambazwa nchi nzima.

"Lengo ni kuwafikia wanawake wote ili hatimaye tuweze kufanikisha azma hiyo ya Mheshimwia Rais Samia Suluhu Hassan," alieleza.

Waziri January alitoa wito kwa taasisi za fedha nchini kuunga mkono jitihada hizo za serikali kwa kuangalia namna zinavyoweza kubuni huduma mahususi za kibenki zinazolenga kurahisisha ununuzi na upatikanaji wa vifaa vya nishati safi ya kupikia.

Akizungumzia dhamira ya Benki ya Exim Tanzania katika kufanikisha mkakati huo, Elizabeth alisema benki hiyo ilitambua kuwa ili kufanikisha azimio la kufikisha asilimia 80 ya wanawake wanaotumia nishati safi nchini, kuna haja kuwainua wanawake kiuchumi ili kuwawezesha kufanya mabadiliko endelevu ya matumizi ya nishati safi.

"Ni kutokana dhamira yetu hiyo ya kumuunga mkono Mheshimiwa Rais Samia, tuliona ipo haja ya kuanza na uwezeshaji wa kiuchumi kwa wanawake ili wawe na nguvu ya kifedha itakayowaongeza kasi na kuwarahisishia mwendo wao kuelekea mabadiliko yanayokusudiwa.

"Na hii ndio sababu kubwa kupitia mafunzo haya tumekuja kuwasilisha huduma zetu mahususi kwa ajili yao ambazo ni akaunti ya SupaWoman na akaunti ya wajasiriamali," alisema.

Akiizungumzia akaunti ya SupaWoman, kiongozi huyo wa benki alisema inalenga kurahisisha uendeshwaji wa biashara miongoni mwa wafanyabiashara wanawake nchini wenye umri kuanzia miaka 18 kwa kuwawezesha kupata mikopo ya dharura ya hadi asilimia 90 ya kiasi kilichopo katika akaunti au hati fungani, mikopo ya nyumba na mikopo ya kawaida ya biashara.

"Pia kupitia akaunti hii, wateja wetu ambao ni wanawake wataweza kupata huduma ya bima ya maisha bure, riba yake inahesabiwa na kulipwa kwa muda atakaochagua mteja mwenyewe, inawawezesha kufanya ununuzi mtandaoni au sehemu yoyote kwa kuwa inawawezesha kufanya miamala kwa urahisi kupitia njia ya simu, mtandaoni au kupitia wakala wa benki yetu," alisema.

Akiizungumzia akaunti ya Wajasiriamali, Elizabeth alisema imeundwa mahususi kwa wamiliki wa biashara ndogo na wajasiriamali, ikilenga kusogeza karibu na kuhamasisha huduma za kibenki kwa makundi hayo muhimu.

"Uwepo wa akaunti hii unalenga kurahisisha uendeshwaji wa biashara miongoni mwa wafanyabiashara wadogo na wajasiriamali wakiwamo mama lishe, wauza chipsi, bodaboda, mafundi, wauza maduka na makundi mengine kwa kuwawezesha kuweka akiba kwa urahisi, kupokea malipo kwa njia za kidijitali sambamba na kuyaunganisha makundi haya na fursa mbalimbali za kibiashara ikiwamo mikopo," alieleza.

# Waomba kupunguziwa gharama ununuzi pembejeo

**Na Maulid Mmbaga**

WAKULIMA mkoani Songwe wameiomba serikali kuwapunguzia gharama za ununuzi wa pembejeo za ruzuku, huku wakieleza kuwa Sh. 70,000 inayotumika kununua mfuko mmoja wa mbolea ni kubwa na kusababisha wengi wao kushindwa kumudu.

Akizungumza na Nipashe jana, mmoja wa wakulima wa maharage mkoani Songwe, Furaha Kibona, mkazi wa Kata ya Ndalambo, mnufaika wa mradi wa Taasisi ya Kuboresha Mifumo ya Masoko ya Kilimo Tanzania (AMDT) wa uhamasishaji wa kilimo himilivu, alisema suala linalowatesa katika kilimo ni uchumi mdogo.

"Kwenye hili la pembejeo tunaiomba serikali itupunguzie kutoka Sh.70,000 tunayonunua kwa kuwa mkulima wa chini hawezi kwenda kununua mbolea kwasababu ya uchumi wake kuwa mdogo, kwahiyo anashindwa kulima kutokana na hilo, serikali itusaidie pembejeo zishuke ili tuweze kumudu," alisema Kibona.

Pia alitoa wito kwa vijana nchini kuachana na kilimo cha mazoea na kufuata maelekezo ya wataalamu ya kilimo bora, akibainisha suala la uhaba wa chakula litakuwa historia nchini endapo watazingatia kilimo himilivu.

Osward Mtindiya, mkulima wa maharage na mmoja wa wanufaika wa mradi wa kilimo himilivu mkoani Rukwa, alisema baada ya kupatiwa mafunzo amebaini kilimo hicho ni kizuri na kimemsaidia kwa kiasi kikubwa kukabiliana na gharama za maisha.

Pia alibainisha kuwa baadhi ya wakulima mkoani humo ni wakwepaji wa gharama zinazohitajika kwenye shughuli za kilimo na kwamba hicho ni moja ya kigezo kinachosababisha waendelee kubaki katika hali ya umaskini, huku akiwasisitiza kufuata elimu ya kilimo bora ili watoke kwenye umaskini.

"Gharama wanazozikimbia wakulima wengi ni katika hatua ya uandaaji wa shamba, ununuzi wa mbegu za kisasa ambazo utofauti wake na zingine zinazaa na zinavumilia mabadiliko ya hali ya hewa.

"Pia katika upandaji kwasababu kunahitajika mtu zaidi ya mmoja, lakini endapo mtu atafuata maelekezo katika mavuno faida atakayoipata ni kubwa kuliko gharama aliyouitumia awali," alisema Mtindiya.

Ofisa ugani kutoka Kampuni ya Ikuo anayehudumu mkoani Songwe, Enosenti Bunga, alisema wamekuwa wakifanya jitihada mbalimbali kwa kushirikiana na AMDT chini ya mradi wa kilimo himilivu katika kuwawezesha wakulima kielimu pamoja na pembejeo zitakazowawezesha katika utekelezaji wa kilimo bora.

Kampuni ya Ikuo yenye makao yake makuu mkoani Rukwa ambayo inajihusisha na biashara ya pembejeo za kilimo na mnunuzi wa mazao ya nafaka kama maharage, pia ni mtekelezaji wa mradi wa kilimo himilivu cha Maharage unaofadhiliwa na AMDT, Mkoa wa Rukwa na Songwe.

"Sisi Ikuo tunatumia mbegu zilizoboreshwa kwa wakulima wetu ambazo zinaendana na hali ya hewa ya aina yoyote pia tuna njia nyingi ambazo tunampa mkulima na mwitikio umekuwa ni mkubwa na tumefikia zaidi ya wakulima 8,000 wanaochukua mbegu kutoka kwetu," alisema Bunga.

Pia alisisitiza serikali kuongeza huduma za ugani kama mabwana shamba katika maeneo mbalimbali ili kuwasaidia wakulima katika masuala yanayohusiana na kilimo.

Bwanashamba kutoka kampuni hiyo, Sumbawanga mjini mkoani Rukwa, Amos Songolo, alisema wanatoa elimu inayowawezesha wakulima kujua namna ya kuandaa shamba, upandaji na utunzaji wa mimea ikiwa shambani, kwa lengo la kumfanya awe mtaalamu na kufanya kilimo chenye tija.

"Kingine tunachokifanya kupitia mradi tunawasaidia wakulima kupima sampuli za udongo, ili ajue anatumia mbolea ipi shambani na kwa kiasi gani kwenye ekari moja, na hilo limeshafanyika na wakulima watapatiwa majibu ili wayatumie kwa msimu unaokuja," alisema Songolo.

Alisema, kutokana na mafunzo waliyoyatoa kumekuwa na mwitikio mkubwa na mpaka sasa wamewafikia wakulima zaidi ya 5,000 ambao wanauhitaji wa mbegu bora.



# Hatima wakurugenzi kusimamia uchaguzi kujulikana kesho

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

KESI ya kupinga wakurugenzi wa halmashauri nchini kusimamia uchaguzi iliyofunguliwa katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ACHPR) na mwanaharakati, Bob Wangwe, akishirikiana na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), uamuzi wake kuanza kutolewa Juni 13, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Msajili wa Mahakama hiyo, Dk. Robert Eno, kesi hiyo ni miongoni mwa kesi tisa zitakazotolewa uamuzi na Mahakama hiyo zikiwamo nane zinazoihusu Tanzania.

Wangwe na LHRC walifungua kesi hiyo baada ya Mahakama ya Rufani nchini, kutengua hukumu ya Mahakama Kuu ya Tanzania iliyokuwa imezuia wakurugenzi wa manispaa, majiji na wilaya kusimamia uchaguzi kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Kesi nyingine zitakazotolewa uamuzi na ACHPR ni kesi namba 7 ya 2016 iliyofunguliwa na Matoke Mwita na wenzake dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na shauri namba 28 la mwaka 2016 la Shija Juma dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Nyingine ni kesi namba 31 ya mwaka 2016, iliyofunguliwa na Umalo Mussa dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kesi namba 32 ya mwaka 2016, iliyofunguliwa na Hoja Mwendesha dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Kesi nyingine ni ya mwaka 2016 iliyofunguliwa na Niyonzima Augustine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na shauri namba 3 la mwaka 2019 lililofunguliwa na Thomas Mgira dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vilevile, liko shauri namba 24 la mwaka 2020, lililofunguliwa na Conaïde Togla Latondji Akouedenoudje dhidi ya Jamhuri ya Benin na shauri namba 39 la 2020 lililofunguliwa na LHRC dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Majaji 11 wa Mahakama hiyo ya Haki za Binadamu na Watu wamechaguliwa kutoka katika mataifa yao kusikiliza mashauri mbalimbali.

## Wafanyabiashara wa mahindi wapewa siku 4 kulipa faini

**Na Mary Mosha,** ROMBO

SERIKALI imetoa siku nne kwa wafanyabiashara wa mazao ya chakula hasa wanaosafirisha mahindi kwenda nje ya nchi kupitia Kituo cha Forodha cha Holili kilichoko Wilaya ya Rombo, mkoani Kilimanjaro, kulipa faini ya kukiuka taratibu za ukaguzi wa ubora na usalama wa chakula.

Hatua hiyo itawawezesha wafanyabiashara hao kuruhusiwa kupitisha mpakani mahindi yao yaliyozuiliwa.

Amri ya kuwatoza faini wafanyabiashara 119 waliokwama kwa wiki ya pili katika mpaka wa Holili unaozitenganisha Tanzania na Kenya, ilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa huo, Nurdin Babu, baada ya kuzungumza na wafanyabiashara hao.

"Kuanzia Juni 10 hadi Juni 13, mwaka huu, wafanyabiashara wote wa mahindi wanaotumia mpaka wa Holili kwenda nchini Kenya kulipa faini. Tumewatoza faini kwa kila lori lenye uzito wa tani kuanzia 10, watalipa Sh. 500,000 na lori lenye tani kuanzia 25, watalipa Sh. 800,000.

"Lakini nawaagiza muache ujanja ujanja, mfuate utaratibu wa kawaida wa kuomba vibali, kabla ya kupeleka mahindi nje ya nchi. Leo nimefika hapa kusikiliza kero zenu, ambazo mlizitoa kupitia vyombo vya habari, ila utafiti zilizofanywa na serikali zinaonyesha kuwa malori ya wafanyabiashara 119 yalikwama kutoka na kukosekana vibali."

Alisema kutokana na wingi wa malori hayo wamelazimika kutoa siku hizo nne ili watendaji wa forodha na Halmashauri ya Wilaya ya Rombo wakamilishe jambo hilo.

"Hili ni onyo la mwisho, hatutawavumilia wafanyabiashara wanaopitisha mizigo yao kinyume na taratibu na kanuni. Sheria inatutaka kutaifisha chakula. Hivyo niwaombe wafanyabiashara kufuata sheria kanuni na taratibu za nchi ili serikali iweze kupata mapato," alisema Babu.

Aidha, Babu alitoa onyo kwa madalali kuacha kuwalaghai wafanyabiashara kwa sababu mbalimbali na badala yake wafuate sheria taratibu na kanuni.

Kabla ya agizo hilo, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Masoko na Usalama wa Chakula wa Wizara ya Kilimo, Aradius Kategeno, alisema wizara hiyo tayari imesitisha vibali vya kusafirisha mahindi nje ya nchi ili kufanya tathmini ya hali ya usalama wa chakula nchini.

"Huu ni utaratibu wa wizara wa kila mwaka, hivyo na kuwaomba wafanyabiashara kusubiri kidogo biashara hiyo wakati serikali zinafanya tathmini kuhusu hali ya chakula.

"Hatutaki wafanyabiashara mje mpate hasara, tunaomba mlielewe hilo, hakuna kibali kitakachotolewa na endapo utasafirisha bila kibali hatua kali za kisheria zitachukuliwa," alisema.

Wakizungumza uamuzi huo baadhi ya wafanyabiashara akiwamo Easter Elisha, alisema uamuzi huo utawasaidia wafanyabiashara kupunguza hasara.

"Tulikuwa na vibali lakini vingine imeisha muda wake tukiwa safarini, tunashukuru serikali ilivyo tusaidia, ila tunaomba tusaidie ili tuweze kuleta na magari mengine yaliyopo njiani.

"Lengo letu sio kukwea kodi, ila bado tunaomba serikali kupunguza vibali na kudhibiti wananchi wanaokwenda shambani na kuchukua mazao ambayo hayajakauka vyema ili kuepusha upatikanaji wa sifa mbaya katika soko," alisema Vailety Antony.




Meneja wa Bank of Africa- Tanzania tawi la Arusha, Kasanga Kaombwe (kushoto), akimkabidhi zawadi ya simu mteja wa benki hiyo, Beatrice Banda, aliyeshinda katika droo ya pili ya kampeni ya fanya mihamala ushinde inayoendeshwa na benki hiyo. Hafla ya kukabidhi zawadi ilifanyika katika tawi la benki hiyo Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Rotary Club yajenga choo kuzuia uchafuzi mazingira

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

TABIA ya baadhi ya wafanyabiashara, abiria kujisaidia ovyo katika kituo cha mabasi Mwika ikilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro imeilazimu Rotary Club ya Mwika kujenga choo cha umma katika eneo hilo ili kuzuia uchafuzi wa mazingira.

Tayari Rotary Club ya Mwika na Serikali ya Kijiji cha Maring'a, Kata ya Mwika Kaskazini, wameingia makubaliano ya kukiendesha kwa tija baada ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa choo cha umma.

Jana Rais wa Club ya Rotary ya Mwika, Mch. Awumsuri Masuki, akizungumza kabla ya kukabidhi choo hicho, alisema hawapendezwi na tabia ya watu kujisaidia haja ndogo katika kituo hicho na wengine kuacha kinyesi, nyuma ya magari au mabasi yanayoegeshwa mkabala na makutano ya barabara kuu ya Mwika/ Rombo/ Himo hadi Soko la Kimataifa la Mwika.


Alisema aibu hiyo imewagusa na kuamua kujenga choo cha umma katika eneo la Mwika Madukani ili kuepusha mlipuko wa magonjwa kama kuhara na kipindupindu kwa walazi wanaoishi jirani na eneo hilo.

"Rotary Club ya Mwika, kwa ushirikiano na Club za Chiko na Moshi, tunakabidhi choo hiki kwa Serikali ya Kijiji cha Maring'a ili kuanza kutoa huduma kwa wapita njia, wapiga debe, wafanyabiashara, wachuuzi na abiria wanaosubiri usafiri. Watu wakija wakisubiri basi pale, wasijifiche nyuma ya gari au basi, si mnawafahamu wanaojificha nyuma ya gari sio!

"Mwenyekiti Kadogoo! Nilikuwa namtania pale, acheni kujificha nyuma ya gari na kujisaidia mikojo. Tunataka wasijifiche nyuma ya gari, waje wajisitiri vizuri hapa (kwenye choo cha umma). Kuna migahawa ya chakula pale, watu wasianze kuhangaika na kwenda shambani, wajisitiri hapa."

Diwani wa Mwika Kaskazini, Samweli Shao, alisema wamepokea choo hicho ambacho sasa ni mali ya wanajamii wote na kwamba ni jukumu lao kama wakazi wa Maring'a kukitunza na kukitumia badala ya kujisaidia nyuma ya magari na migomba.

Alisema: "Naagiza kuanzia sasa wananchi wa Maring'a asitokee mtu anayefikiri kuuhujumu mradi huu, tuutunze na kuutumia vyema kwa mujibu wa kanuni za afya ili tuepuke magonjwa ya mlipuko ambayo ni hatari."





# Kampuni yajenga shule kudhibiti mimba za utotoni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

UJENZI wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Bulyanhulu iliyopo Kata ya Bulyanhulu Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, imetajwa itakuwa msaada wa kupunguza tatizo la mimba za utotoni.

Mkuu wa shule hiyo ambayo ni ya bweni, James Mukasa, alibainisha hayo juzi wakati wa ziara ya waandishi wa habari waliotembela miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo imetekelezwa na kampuni ya uchimbaji madini ya dhahabu ya Barrick kupitia mgodi wake wa Bulyanhulu.

"Baadhi ya wanafunzi wanaosoma katika shule mama ya Sekondari ya Kata Bulyanhulu baadhi yao wanatoka umbali mrefu zaidi ya kilomita 14 hadi 15, hali inayosababisha wanafunzi wa kike kurubunika na kuangukia kwenye mapenzi, hivyo shule ambayo itakuwa na bweni itasaidia kudhibiti kero hiyo," alisema Mukasa.

Kaimu Meneja Uhusiano ya Jamii mgodi wa Bulyanhulu, Zuwena Senkondo, alisema ujenzi wa shule hiyo ulianza mwaka 2021 na utakamilika mwaka huu, kwamba mwakani itaanza kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza, imegharimu zaidi ya Sh. milioni 800.

Alisema shule hiyo itakuwa ya vipaji maalumu na ina maabara zote za sayansi, kwamba itasaidia taifa kuwa na wataalamu wake wa ndani.

# Jeshi la Polisi lawaita wanaume wanaofanyiwa ukatili

**Na Shabani Njia,** KAHAMA

JESHI la Polisi wilayani Kahama kupitia dawati la jinsia na watoto limewashauri wanaume wanaofanyiwa vitendo vya ukatili ndani ya familia zao kuripoti katika kituo cha polisi kwa ajili ya kupata msaada.

Limesema waache kuyafumbia macho kwa kuogopa aibu huku wakiendelea kuumia ndani ya mioyo yao.

Ofisa wa Jeshi la Polisi kutoka dawati hilo, Joyce Godlizen, aliyasema hayo wakati wa kilele cha Siku ya Hedhi Salama Duniani iliyofanyika katika Kata ya Kagongwa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.

Alisema wapo tayari kutunza siri zote kuhusu matatizo ambayo yatakuwa yameelewa na mwanaume na siyo vinginevyo.

Alisema dawati hilo lipo kwa ajili ya kupokea malalamiko kutoka makundi ya jinsi yote ikiwamo ya wanaume ambao wamekuwa wakifanyiwa vitendo viovu ndani ya ndoa na familia zao lakini wanakaa kimya kwa kuogopa kuchekwa.

Katibu wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Wilaya ya Kahama, Happynes Mpela, alisema maadhimisho hayo yameambatana na utoaji wa elimu ya hedhi salama pamoja na madhara endapo wanafunzi watatumia vitu ambavyo siyo salama kwao ikiwamo vitambaa na magazeti. Naye Ofisa Tarafa wa Msalala, Victoria Lusana, alisema, wanafunzi wanaoishi katika mazingira magumu wamekuwa wakikabiliwa na matatizo mengi ikiwemo ya ukosefu wa taulo za kike na kulazimika kuingia kwenye vishawishi vya kufanya ngono kwa lengo la kutafuta mahitaji.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi hao, Janeth Julius alishukuru kupata taulo hizo ambazo zitawasaidia kujikinga na maradhi yatokanayo na uchafu.

Alisema wamekuwa wakitumia vitambaa, vidaso, vipande vya godoro na magazeti kujikinga na hedhi na wakati mwingine wanakosa masomo.



Mkuu wa Shule ya Sekondari Kata ya Bulyanhulu Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, James Mukasa, akionyesha viti na meza 320 ambavyo vitatumiwa na wanafunzi wa kidato cha kwanza mwakani katika shule mpya ya sekondari ya wasichana ya vipaji maalum ambayo imejengwa na kampuni ya Barrick Bulyanhulu kwa zaidi ya Sh. milioni 800. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Bil. 12.7/- kudhibiti uchafuzi Ziwa Victoria

**Na Vitus Audax, MWANZA**

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) imepokea Sh. bilioni 12.7 kwa ajili ya upanuzi wa mtandao wa majitaka, lengo likiwa ni kudhibiti uchafuzi wa mazingira katika Ziwa Victoria.

Inaelezwa kuwa tatizo la uchafuzi wa mzingira katika Ziwa Victoria pamoja na maeneo mengineyo katika Mkoa wa Mwanza husababishwa zaidi na wakazi wa maeneo ya milimani ambao hufungulia chemba za vyoo nyakati za mvua.

Akizungumza na Nipashe juu ya hali ya uhifadhi wa Ziwa Victoria, Ofisa Uhusiano kwa Umma kutoka Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria (LVBWB), Mhandisi Gerald Itimbula alisema kuwa hakuna kiwanda chochote wala taasisi inayotiririsha maji taka ambayo hayajatibiwa katika Ziwa Victoria.

Alieleza kuwa kila kiwanda na taasisi hutibu maji taka yake na kabla ya kuruhusiwa kuelekea ziwani, hupimwa na maabara ya bodi hiyo ili kujiridhisha kama kiwango cha uchafu wake kunaruhusiwa kuingia ziwani.

"Kilichobaki kwa sasa ni wale wananchi wanaotiririsha maji taka hususani katika kipindi cha mvua lakini zipo hatua za utekelezaji wa mradi mkubwa kupitia MWAUWASA utakaodhibiti kwa kiasi kikubwa kero hiyo," alieleza Mhandisi Itimbula.

Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira kutoka MWAUWASA, Mhandisi Salim Lossindilo, alieleza Nipashe kuwa katika mwendelezo wa kudhibiti tatizo hilo Novemba 23,2022 walisaini mkataba wa Sh.bilioni 12.7 kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu ya majitaka katika maeneo ya Ilemela na Jiji la Mwanza.

"Kwa sasa kazi ya kuhuisha usanifu wa mradi inaendelea na itakapokamilika taratibu za manunuzi ya mkandarasi zitafanyika ikiwa matarajio ni kuanza kazi za ujenzi mapema mwaka 2024 ambao unatarajiwa kukamilika mwaka 2026," alisema Mhandisi Lossindilo.

Mhandisi Mkuu na Mratibu wa Miradi inayotekelezwa kupitia Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria kutoka Wizara ya Maji, Mhandisi Abdullah Matata alisema mradi huo unatarajiwa kuwafikia wananchi kutoka kaya 1,600.

Alitaja maeneo korofi yatakayofikiwa na mradi huo kuwa ni Kirumba, Pasiansi, Kitangiri, Nyamanoro, Igogo pamoja na maeneo ya milimani Ilemela.

"Fedha za kutekeleza mradi huo zimetolewa na wadau wa maendeleo kutoka Umoja wa Ulaya (EU) pamoja na Serikali ya Ujerumani na kutekelezwa kupitia Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW) kupitia Kamisheni ya Bode la Ziwa Victoria Afrika Mashariki ukiwa ni miongoni mwa miradi inayoratibiwa katika maeneo ya Kisumo (Kenya) , Kigali (Rwanda), Mwanza , (Tanzania) ,Kampala (Uganda) pamoja na Burundi.

Wakieleza kero ya hiyo ya muda mrefu baadhi ya wakazi wanaoishi kando ya Ziwa Victoria wakiwamo wavuvi walisema nyakati za mvua wamekuwa wakishuhudia utiririsha wa maji taka katika maeneo ya makazi yao, huku wengine wakimwaga uchafu huo kuelekea katika mitaro inayopeleka maji Ziwa Victoria.

Mmoja wa wavuvi, Emmanuel Kisinda alisema: "Maji taka yanayoelekezwa ziwani yamesababisha kuhama kwa samaki na kuelekea katika kina kirefu hali inayosababisha wavuvi kutumia gharama kubwa ya mafuta kupata."

Nipashe
Spotika



HAZARD NA FUNGU LA KUKOSA REAL MADRID UK. 12-13


ZAHA

# WACHEZAJI 6 HURU AMBAO MAN UNITED INAWEZA KUWAPATA

## ISIKUPITE

BEKI Mwingereza Harry Maguire anaweza akaikosesha nafasi klabu yake ya Manchester United kumsajili beki wa kati wa Napoli raia wa Korea Kusini, Kim Min-jae (26), kama Mwingereza huyo atakataa ombi la klabu hiyo la kumtaka aondoke Old Trafford, mchezaji huyo tayari ameonyeshwa mlango wa kutokea ili kuipa nafasi klabu hiyo kusajili beki mwingine.



**MANCHESTER,** England

AWAMU ya kwanza ya ujenzi wa kocha, Erik ten Hag katika timu ya Manchester United ulikwenda vizuri sana.

Raia huyo wa Uholanzi alirekebisha vizuri kikosi na kuingiza mtindo wa uchezaji wa kuvutia ambao ulileta matokeo thabiti, lakini bado kuna kazi ya kufanywa katika dirisha la usajili la majira ya joto na linawakilisha fursa nzuri ya kuendelea kukijenga kikosi.

Huku wengi wakiwa wanapatikana kwa bei ghali, Man United inaweza kulazimika kuwa wabunifu kidogo wanapotafuta kuziba baadhi ya mashimo kwenye kikosi chao. Kwa kuzingatia hilo, hapa kuna baadhi ya wachezaji 6 ambao wapo huru na Man United wanapaswa kuwaangalia ili kuokoa fedha.

### 1. Marcus Thuram - Borussia Monchengladbach

Mpango wa Man United wa kupata mshambuliaji mpya limekuwa jambo la wazi kwa muda mrefu. Anthony Martial sio mtu wa Ten Hag na mkopo wa Januari wa Wout Weghorst pia haukuweza kutatua tatizo.

Harry Kane, ambaye anaonekana kutoweza kufikiwa, na wachezaji wawili wa bei ghali Victor Osimhen wa Napoli na Randal Kolo Muani wa Eintracht Frankfurt wote wanazingatiwa, lakini kuna mfungaji aliyethibitishwa uwezo wake anayesubiri kusajiliwa bila malipo, Marcus Thuram.

Thuram anayecheza kama winga, alifunga mabao 16 na asisti saba katika mashindano yote. Ongeza kwa hakika ana umri wa miaka 25 tu na utaona ni kwa nini timu nyingi kubwa za Ulaya zinamfuatilia Mfaransa huyo.

### 2. Stefan de Vrij - Inter Milan

Inter Milan wamekuwa wakijaribu kumfunga beki wa kati wa Uholanzi, Stefan de Vrij kwa mkataba mpya kwa miezi kadhaa, lakini kwa sababu yoyote ile, bado wanasubiri.

Akiwa na umri wa miaka 31, De Vrij anaweza kutokuwa chaguo la muda mrefu kwa Man United, lakini anaweza kuwa mchezaji mwenye uzoefu ili kuwasaidia, Lisandro Martinez na Raphael Varane, huku akimruhusu mmoja kati ya Victor Lindelof au Harry Maguire kuondoka klabuni hapo.

Akiwa na takriban mechi 500 za kiwango cha juu kwa jina lake, De Vrij analeta hekima na uzoefu, na hilo linaweza kuwa kubwa kwa Mholanzi mwenzake Ten Hag anapoendelea kujenga utamaduni mpya pale Old Trafford.

### 3. Evan Ndicka - Eintracht Frankfurt

Ikiwa Ten Hag anapendelea kuimarisha safu yake ya nyuma, hatapata bora kwenye kundi la wachezaji waliopo huru kama Evan Ndicka.

Akiwa na umri wa miaka 23 pekee, Ndicka alikaribia kucheza mechi 200 akiwa Frankfurt kabla ya kuchagua kupeleka kipaji chake kwingine msimu huu wa joto. Haishangazi, kuna klabu nyingi zinazomtaka beki huyo ambaye uwezo wake wa mguu wa kushoto unamfanya kuwa wa thamani zaidi.

Ikiwa yuko tayari kwa jukumu la kuanza mara moja au la ni mjadala, lakini Ndicka anaonekana kama nyota anayesubiriwa na Man United ingekuwa busara wangejitosa kumnasa.

### 4. Youri Tielemans - Leicester

Uzoefu wa kwenye Ligi Kuu ya England unaonekana kuwa wa thamani zaidi katika mchezo wa leo, wakati bidhaa ghali kutoka nje zinaposhindwa kuzoea maisha ya ligi hiyo.

Ingawa wakati wa Youri Tielemans ulimalizika kwa dosari mbaya, ni wachache ambao wanaamini kuwa kuanguka kwake na Leicester ni onesho la kipaji chake.

Wakati Leicester City walipokuwa kwenye kiwango bora miaka michache iliyopita, Tielemans alionekana kama mmoja wa viungo bora katika kitengo hicho. Inaweza kuwa hatari kidogo kumchukua, lakini ikiwa kujiamini ndiko kulikokosekana kwenye mchezo wake, basi anaweza kuisaidia klabu hiyo. Unaweza kumuita Christian Eriksen mdogo.

### 5. Adrien Rabiot - Juventus

Adrien Rabiot amegawanyika kimaoni katika klabu ya Juventus. Ingawa wengine wametilia shaka uthabiti wake, wengine wameelekeza sura yake ya nyati na uwezo wake wa kubeba mpira kwa kipaji chake maalum alichokuwa nacho mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28.

Akiwa na kiwango kizuri zaidi cha ushambuliaji, Rabiot anaweza kufunga mabao na kuwatengenezea wale wanaomzunguka. Anapopata nafasi yake, ni vigumu sana kusimama - tofauti na kiungo mwingine Mfaransa ambaye alikuwa akiita Old Trafford nyumbani.

United wanahitaji usaidizi katika eneo la kiungo na uhamisho wa Marcel Sabitzer wa Januari ulipaswa kuongeza ustadi na makali kwenye eneo hilo la uwanja. Kuchukua nafasi kwa Rabiot kunaweza kuwa nafasi nzuri zaidi.

### 6. Wilfried Zaha - Crystal Palace

Wilfried Zaha, kama United tayari wanajua, ni fowadi hodari ambaye anaweza kucheza popote katika safu ya ushambuliaji na anajua jinsi ya kuleta mabadiliko ya kweli katika Ligi Kuu ya England.

Anaanza na Marcus Rashford? Hapana. Je, anaweza kuwasaidia Jadon Sancho, Antony na Alejandro Garnacho kukua hadi kufikia kiwango cha juu zaidi katika uchezaji wao kama nyota wasaidizi? Kwa uhakika kabisa.

## Extra Time




H AZARD

# HAZARD NA FUNGU LA KUKOSA REAL MADRID

**MADRID,** Hispania

UHAMISHO wa Eden Hazard kwenda Real Madrid mwaka 2019 ulionekana kama uhamisho ambao ungefanya kazi kwa pande zote mbili.

**Baada ya kuwa na muda wa kuvutia sana kule London Magharibi akiwa na Chelsea, akishinda mataji mawili ya Ligi Kuu ya England, Ligi ya Europa na mataji zaidi ya nyumbani, nyota huyo wa Ubelgiji alikubali kuhamia pale kwenye Uwanja wa Bernabeu kwa ada kubwa ambayo ingeweza kupanda hadi pauni milioni 150.**

Alijiondoa katika soka la Uingereza kama mchezaji bora wa Ligi Kuu ya kisasa na alifika Hispania kwa shangwe nyingi.

Lakini badala yake uchezaji wa Hazard katika mji mkuu wa Madrid ukawa mbaya tofauti na matarajio.

Na hatimaye Real Madrid imechagua kusitisha mkataba wake msimu huu wa joto wa 2023.

Hiyo ni mwaka mmoja kabla ya mkataba wake wa awali kumalizika na kumuacha Hazard akiwa na mechi 76, mabao saba na mataji kadhaa baada ya misimu yake minne akiwa na klabu hiyo.

### MAJERAHA

Majeraha yakawa adui mbaya zaidi kwa Hazard pale Hispania, jambo ambalo lilishangaza kwani alikuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu sana.

Tofauti ya wakati uliotumika na ule aliokaa nje ya uwanjani ilikuwa kubwa mno.

Kwa miaka saba aliyoitumikia The Blues, fowadi huyo alikosa jumla ya michezo 21 tu, lakini pale Hispania amekosekana kwa mechi 78 katika kipindi chake cha miaka minne nchini Hispania.

Mbelgiji huyo amekuwa akiuguza majeraha ya misuli ya hapa na yalimfanya akose kucheza, huku nyota wachanga na waliopatikana kwa urahisi wakianza kung'ara kwenye uwanja wa Bernabeu.

### KUIBUKA NYOTA WADOGO

Hebu fikiria kujaribu kuweka msumari mahali pa kuanzia wakati shindano la haraka la kukimbia.

Vinicius Junior, ambaye bila shaka ni mmoja wa wachezaji anayesisimua zaidi ulimwenguni hivi sasa.

Mbrazili huyo alicheza kila wiki katika msimu wa 2022/23 baada ya kuwa nyota wa msimu uliopita na kumuacha Hazard akikosa nafasi ya kurudi uwanjani.

Wachezaji kama Rodrygo na Federico Valverde pia wamefurahia muda mwingi wakati Hazard akizidi kukaa nje kwa majeruhi.

Huku ujenzi ukiendelea kupamba moto msimu wa majira ya joto 2023, hakukuwa na sababu ya kumbakisha Hazard huku wachezaji wa kusisimua kama hao wakiwepo na hivyo kuchagua kumwacha mchezaji huyo wa zamani wa Lille ili akatafute changamoto mpya sehemu nyingine.

### VIWANGO VYA JUU

Kama ilivyo kwa timu kubwa za Ulaya Real Madrid ni klabu iliyoundwa na washindi.

Wamesajili mara kwa mara na kutoa wachezaji wenye uwezo wa kiakili kufanya kile kinachotakiwa uwanjani.

Labda kuonesha kipaji chake Hazard kule London kunaweza kulihusishwa na uchezaji wa Chelsea unaomzunguka kama nyota mkuu, wakati alikuwa mchezaji mwingine tu katika orodha ya Los Blancos. Hilo halihusu kidogo kipaji chake cha asili, lakini kwa hakika Hazard ameshindwa kufikia viwango vilivyowekwa na Real Madrid.

Pia alipewa jukumu kubwa la kuchukua jezi namba saba, ambayo hapo awali ilivaliwa na Cristiano Ronaldo.


Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno ndiye aliyekuwa chanzo kikuu cha mabao kwa Real katika miaka yake ya kuitumikia klabu hiyo na historia yake imefuatwa na mchezaji ambaye alifunga wastani wa kufunga kila mechi 11.

Madrid wangeweza kumsaidia Hazard kwa kuelewa kwamba hakuwa mchezaji kama Ronaldo na hangeweza kufikia viwango hivyo vya juu vya mabao ambavyo Real Madrid ilivitaka.

Ikiwa mchezaji hawezi anakumbwa na majeraha na masuala ya utimamu wa mwili, ni vigumu timu kumbakiza kwa timu kama Real Madrid.

## Nukuu

"Kwanza kabisa maneno yangu ya kwanza ni kwa Inter, nawapongeza kwa uchezaji wao, pili kwa mkurugenzi wangu wa michezo, Mkurugenzi Mtendaji na mwenyekiti wangu, kwa kawaida usiposhinda Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya miaka mingi unafukuzwa, hapa wamenivumilia na leo hii tumefanikiwa kuchukua ubingwa wa Ulaya," **Kocha wa Manchester City Pep Guardiola akizungumzia ubingwa wa Ulaya walioutwaa juzi usiku.**



"Nimekuwa kwenye soka kwa muda mrefu, naweza kusema Guardiola (Pep) ni kocha bora wa muda wote Ulaya, wapo wengine wanaweza wakawa na maoni sawa na mimi", **Mshambuliaji wa zamani wa Arsenal, Barcelona na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Thierry Henry akimzungumzia Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.**



"Ni usiku wa kukumbukwa, uliojaa hamasa na msisimko, furaha yangu haielezeki baada ya kufanikiwa kuchukua ubingwa huu, hizi ni juhudi zetu wote, wachezaji, makocha na viongozi," **Rodri, nyota wa Manchester City akizungumzia ubingwa wao wa Ulaya.**





# WAMEVUNA WALICHOPANDA LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

SAFARI ndefu ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/23 ilitamatika Ijumaa iliyopita, wakati timu zote 16 zilipomalizia raundi ya 30 na kukaa pale zilipostahili.

Ligi hiyo iliyoanza Agosti 15, mwaka jana, ilihitimishwa kwa bingwa Yanga kukabidhiwa 'mwali' wao mpya aliyetambulishwa na wadhamini wa Ligi Kuu hivi karibuni.

Baada ya ligi kumalizika, kila timu imevuna ilichopanda, kwani kila iliyofika kwenye nafasi iliyopo, ndiyo mavuno ya msimu mzima kwa jinsi ilivyojiandaa.

Ukiacha ubingwa, kuna timu zilizopata tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika, Kombe la Shirikisho, zilizosalia na zile zitakazokwenda kucheza mchujo 'play off' na zipo pia ambazo tayari zimeipa mkono wa kwa heri ligi hiyo, hivyo kutoonekana tena msimu ujao.

Mwandishi wa makala haya amechambua ushiriki wa timu zote kwenye ligi hii msimu mzima.

**1. Yanga**

Haikushangaza sana kutwaa tena ubingwa kwa mara ya pili kutokana na viwango vya wachezaji wao, upambanaji, kujituma, mbinu za kocha wao Mtunisia Nasreddine Nabi, pamoja na kuwa na kikosi kipana.

Yanga ni moja kati ya timu chache kwenye Ligi Kuu iliyokuwa na wachezaji wenye viwango vinavyofanana wale wanaokuwa uwanjani na wanaokuwa benchi.

Hata hivyo kuna sehemu ambayo wengi wanairuka na kutoipa pongezi, nayo ni eneo la kocha wa viungo wa timu hiyo. Yanga imetwaa ubingwa na kufika hata kwenye fainali ya Kombe la Shirikisho kutokana na pia na ufiti, au utimamu wa mwili wa wachezaji wake ambao karibia wote wanaoanza na walio benchi walionekana wako timamu kimwili hata pumzi. Msimu huu imetwaa ubingwa ilimaliza na pointi 78, nne zaidi ya msimu uliopita ilipomaliza na pointi 74.

**2. Simba**

Kuna vitu vichache tu ambavyo vimeifelisha Simba msimu huu. Ukiangalia takwimu karibia zote zinawabeba. Imefunga mabao 75 ambayo ni mengi zaidi kuliko timu yoyote, ikiruhusu mabao 17, machache zaidi kuliko timu zote. Hata pointi ilizomaliza nazo ni 73, ambazo ni 12 zaidi kuliko za msimu uliopita ilipomaliza na pointi 61 tu.

Ufinyu wa kikosi kwa kiasi kikubwa wa uliinyima ubingwa, kwa sababu ilikuwa na wachezaji wa kikosi cha kwanza tu, wachezaji wa benchi hawakuwa na viwango vinavyokaribiana na wale anaoanza .

Wachezaji Joash Onyango na Clatous Chama kwa nyakati tofauti pia wazilitaja mechi dhidi ya Azam ya mzunguko wa kwanza waliopoteza kwa bao 1-0 na sare ya mabao 2-2 dhidi ya KMC ilizitoa timu hiyo kwenye reli. Faraja pekee ni kwamba imepata tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

**3. Azam FC**

Imekamata nafasi ya tatu kama kawaida yake, safari hii ikikusanya pointi 59, ambazo ni 10 zaidi ya zile za msimu uliopita ilipomaliza na pointi 49. Imefanikiwa kukata tiketi ya kucheza mechi za Shirikisho la Soka Afrika msimu ujao, zaidi ya hapo haikuwa na cha ajabu sana zaidi ya ilivyokuwa kwenye misimu iliyopita.

**4. Singida Big Stars**

Ni timu iliyoanza kucheza Ligi Kuu msimu huu na moja kwa moja inakwenda kushiriki Kombe la Shirikisho barani Afrika, pamoja na hayo, matokeo mazuri iliyokuwa inayapata hayakuwashangaza mashabiki wa soka kutokana na aina ya wachezaji iliyokuwa nayo, na wale ambao imewasajili baadhi wameonyesha uwezo mkubwa na wengine ni wazoefu kutoka klabu kubwa, husussan Simba na Yanga.

**5. Namungo FC**

Imemaliza kwenye nafasi ya tano kama ilivyokuwa msimu uliopita. Hata hivyo msimu huu imepungua kasi, kwani imemaliza mechi 30 ilipata pointi 40, wakati msimu uliopita ilimaliza idadi ya mechi hizo ikiwa na pointi 41.

Baada ya kutofanya vema msimu uliopita, ilitegemewa msimu huu ingekuwa na nguvu mpya, lakini iliendelea kuwa ni ile ile ya msimu iliopita na si ya kutisha kama misimu miwili nyuma.

**6. Ihefu SC**

Hii ni moja kati ya timu iliyowashangaza mashabiki wengi wa soka. Imepanda daraja msimu huu, baada ya kuteremka msimu wa 2020/21.

Hadi mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu unamalizika ilikuwa inahesabika kuwa itakuwa moja ya timu zitakazoshuka daraja hata hivyo ilibadilika na kuwa tishio mzunguko wa pili hasa baada ya kupata wachezaji wa mkopo kutoka klabu za Simba na Yanga, hadi kumaliza ikiwa katika nafasi ya sita.

Kwa maana hiyo msimu huu hakuna timu iliyopanda na kushuka moja kwa moja.

**7. Geita Gold**

Haikuwa kama ile ya msimu uliopita iliyomaliza wa nne na kucheza Kombe la Shirikisho barani Afrika, haikuwa na msimu mzuri sana hivyo imemaliza ikiwa ya katika nafasi ya saba, ingawa haikuwa na tishio lolote la kutaka kushuka daraja.

Ilichanga karata zake vizuri na ikawa kwenye nafasi ya katikati ya msimamo kwa muda wote wa ligi.

**8. Prisons**

Msimu uliopita ilinusurika kwenye mechi za mchujo 'play off', inaonekana kuwa somo liliwaingia. Hata hivyo, mpaka mzunguko wa kwanza unamalizika ilikuwa hoi bin taaban. Ilibadilisha nafasi ya Ihefu kule mkiani.

Wakati Ihefu ikishtuka mapema mwanzoni tu mwa mzunguko wa pili, Prisons ilianza kugangamala katikati ya mzunguko huo, hasa baada ya ujio wa Kocha Mohamed Abdallah 'Bares' na kuifanya kumaliza nafasi ya nane kwa pointi 37, badala ya nafasi ya 14 msimu uliopita ikimaliza na pointi 29.

**9. Dodoma Jiji**

Ni moja kati ya timu iliyojifunza kutokana na makosa ya msimu uliopita. Japo haikuwa kwenye nafasi nzuri sana, lakini imemaliza ikiwa ya tisa, ikikusanya pointi 37 na kuwa na uhakika wa kubaki Ligi Kuu. Msimu uliopita ilimaliza ya 11, na pointi 35.

**10. Mtibwa Sugar**

Inaonekana kama ni timu iliyozoea kuzicheza karata zake vema kwenye mechi za mwisho. Msimu uliopita iliponyeka kwenye 'play off' dhidi ya Transit Camp, ikifungwa bao 1-0 ugenini, na kushinda 4-1 nyumbani.

Ilimaliza nafasi ya 13 ikiwa na pointi 31. Msimu huu, pamoja na kwamba ilikuwa kwenye hali mbaya, lakini ilimaliza nafasi ya 10, pointi 35.

**11. Kagera Sugar**

Haikufanya vema msimu huu. Imemaliza nafasi ya 11 na pointi zake 35, wakati msimu uliopita ilimaliza ya sita, ikiwa na pointi 39.

**12. Coastal Union**

Imeponea chupuchupu kucheza 'play off' kama ilivyokuwa msimu uliopita iliponusurika dhidi ya Pamba FC. Safari hii imemaliza nafasi ya 12 na pointi 33.

**13. KMC**

Inawezekana tukawa nayo msimu ujao au la, Imeshika nafasi ya 13 kwenye msimamo na itakwenda kucheza 'play off' dhidi ya Mbeya City. Msimu iliopita ilimaliza kwenye nafasi ya 10.

**14. Mbeya City**

Kwa miaka ya karibuni imekuwa ni timu ya kusuasua kutoka kuwa tishio, nayo itajaribu bahati yake dhidi ya KMC kwenye mechi ya 'play off'.

Angalau msimu uliopita ilimaliza nafasi ya tisa na pointi 37.

**15. Polisi Tanzania**

Wala haikushangaza yoyote ilivyoshuka daraja, ilionekana tangu mwanzo kuwa safari ingewakumba.

Imemaliza ligi ikiwa na pointi 25 tu, wakati msimu uliopita ilimaliza kwenye nafasi ya nane ikiwa na pointi 37.

**16. Ruvu Shooting**

Ndiyo timu ya kwanza kushuka daraja msimu huu, kama alivyosema kocha wake mkuu Mbwana Makata aliyejiunga baadaye sana kwenye kikosi hicho kuwa tatizo lilianza kwenye usajili.

Haikuwa na wachezaji wenye viwango na hata wakati wa dirisha dogo hakukuwa na fungu la usajili kiasi cha kuongeza mchezaji mmoja tu. Msimu uliopita ilishika nafasi ya 12.

**JE, WAJUA?**



MANCHESTER City imekuwa klabu ya pili nchini England kutwaa makombe yote matatu katika msimu mmoja, kombe la FA, Kombe la Ligi Kuu na Kombe la Klabu Bingwa Ulaya, Manchester United ilikuwa timu ya kwanza kufanya hivyo mwaka 1999.



# TRA Mkalama yavuka lengo ukusanyaji mapato

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MKALAMA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Wilaya ya Mkalama mkoani Singida imevuka lengo la ukusanyaji mapato kwa kukusanya Sh. milioni 277, lengo kuu lilikuwa ni kukusanya Sh. milioni 250 kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 mamlaka hiyo hadi Mei 31, mwaka huu imekusanya Sh. milioni 611 kati ya lengo la kukusanya Sh. milioni 700.

Meneja wa TRA Wilaya ya Mkalama, Iddy Omary, alisema hayo juzi katika kikao cha Kamati ya Ushauri wa Kodi Wilaya.

Kikao hicho wajumbe walikuwa na lengo la kupitia utendaji wa kazi wa mamlaka hiyo na kutoa dira juu ya hali ya biashara na ukusanyaji mapato wilayani humo.

Omary alisema kwa mwaka wa fedha 2023/2024 TRA wilayani humo imejipanga kukusanya Sh. bilioni 1.5 ambapo makusanyo hayo yatafikiwa kutokana na mkakati uliowekwa na mamlaka hiyo wa kutoa mafunzo ya kuwajengeza uwezo pamoja na kuendelea kutumia mashine za kielektroniki katika kutoa risiti. Naye Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Moses Machali, alipongeza TRA kwa ukusanyaji wa mapato na kuvuka lengo na kuwataka wafanyabiashara kulipa kodi kwa uaminifu kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Machali alisisitiza uwapo wa ushirikiano baina ya TRA na Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA), Halmashauri ya Wilaya pamoja na taasisi zote wilayani hapa ili kuongeza ukusanyaji wa mapato. Hivyo, aliitaka kamati kuhakikisha kila mmoja kwa nafasi yake anasimamia suala hilo kikamilifu kwa maendeleo ya wananchi.

Katika hatua nyingine Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) wilayani Singida limetakiwa kuwa kiunganishi kizuri kati ya wafanyabiashara na serikali ili kupunguza matatizo yanayowakabili wafanyabiashara katika wilaya hiyo.

Mwenyekiti wa baraza hilo ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Paskas Mulagiri, akizungumza kwenye kikao cha baraza alisisitiza wafanyabiashara kulipa kodi na ada kupitia mifumo ya serikali ya ulipaji na kupatiwa risiti za kielektroniki.

Muragili alisema TCCIA linapaswa kuwa kiunganishi kati ya serikali na sekta binafsi katika masuala yote yanayohusu biashara ili kutatua matatizo yanayowahusu wafanyabiashara.

Pia aliitaka Manispaa ya Singida kuboresha mfumo wa kutoa elimu kwa ngazi zote kuhusu tozo mbalimbali kwa wafanyabiashara ili kuepuka migogoro.



Mkuu wa Kanda ya Kati wa Vodacom Tanzania PLC, Joseph Sayi (kushoto), akiwakabidhi zawadi ya mabegi wanafunzi waliofanya vizuri wakati wa kufunga mafunzo ya wiki moja ya kuwajengea uwezo wa masomo ya TEHAMA wanafunzi wa kike yaliyofanyika jijini Dodoma kwa kushirikiana na Tanzania Data Lab (dLab) yajulikanayo kama 'Code Like a Girl' yaliyokamilika mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICGA WETU**

# Mchakato ununuzi meli za uvuvi waiva

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonaz, amesema serikali imetia saini mkataba wa kufanya tathmini ya athari ya kimazingira na kijamii kwa ajili ya ununuzi wa meli za uvuvi, kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP).

Akizungumza juzi baada ya kutia saini mkataba huo, alisema kuwa mkataba huo utawezesha kufanyika kwa tathmini ya athari ya mazingira pamoja na matengenezo ya meli zitakazotumika katika uvuvi wa bahari kuu ili kupata mazao yatakayochangia uchumi wa nchi.

Dk. Yonaz alisema kuwa sambamba na tathmini hiyo pia kutafanyika upembuzi yakinifu katika kuundwa kwa vyombo hivyo, kazi itakayofanyika kwa siku 75 ambapo itagharimu Sh. milioni 349.

Alisema kuwa Tanzania inazo rasilimali nyingi za majini hivyo ili kuinua uchumi kupitia uchumi wa buluu serikali imeona ni muhimu kutengeneza meli kubwa zitakazovua katika kina kirefu kwa ajili ya kupata mazao ya baharini.

"Mwaka huu meli nne zitatengenezwa kwa ajili ya Zanzibar na meli tano kwa ajili ya Tanzania Bara, hivyo kukamilika kwa meli hizo kutasaidia kuinua uchumi wa pato la taifa," alisema Dk. Yonazi.

Pia aliwahimiza wadau wa uvuvi ambao ni Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) na Shirika la Uvuvi la Zanzibar (ZAFICO) kushirikiana na mkandarasi huyo kuhakikisha kazi hiyo inafanyika kikamilifu, huku akihimiza kila mmoja kuwajibika kwa sehemu yake kwa lengo la kupata matokeo chanya.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Ushauri wa Masuala ya Mazingira (TANSEQ), Lusako Raphael, amebainisha kuwa lengo la kufanya tathmini hiyo ni kuhakikisha mradi hausababishi athari hasi katika mazingira na jamii.

Alisema mradi huu unalenga kuwezesha ununuzi wa meli pamoja na uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata samaki, hivyo wanategemea kupata ushirikiano kutoka kwa TAFICO, ZAFICO na Wizara ya Kilimo.

Alisema serikali imeweka mkakati wa kudhibiti athari za mazingira ambao ndiyo utakuwa mwongozo wa utekelezaji wa mradi.

# Diwani ashtakiwa kwa kuwashawishi wananchi kugoma

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

DIWANI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Mitundu Halmashauri ya Itigi wilayani Manyoni, Patrick Masanja, ameshtakiwa kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, kwamba amekuwa kikwazo cha utekelezaji wa miradi katika kata hiyo, anawashawishi wananchi wagome kushiriki nguvu kazi.

Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Kemilembe Lwota, juzi alimweleza Serukamba kwamba diwani huyo kwa muda mrefu amekuwa akiwashawishi wananchi wasishiriki kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa na kituo cha afya.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa huyu diwani ni tatizo wala siyo kwa suala la hapa shuleni, amekuwa tatizo kwa muda mrefu kwa kuwashawishi wananchi wasishiriki kwenye ujenzi miradi ya maendeleo na amekuwa akifanya hivyo sababu anaona hachukuliwi hatua zozote na anaona mambo yanakwenda tu," alisema.

Lwota alisema hivi karibu akiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya walifika katika kata hiyo kushughulikia mgogoro wa mnada ili uweze kuhamishwa, kupelekwa eneo jingine lakini diwani huyo hakuzungumza chochote wala kutoa ushirikiano kwenye mkutano na badala yake yeye na wananchi wake waliamua kuondoka kabla mkutano haujaisha.

Alisema Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya ya Manyoni ilifanya ziara hivi karibu katika Kata ya Mitundu lakini diwani huyo aligoma kushiriki ziara hiyo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Itigi, John Mgalula, alisema diwani huyo amekuwa kikwazo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kusababisha baadhi ichelewe kukamilika kutokana na kukosekana kwa nguvu kazi ya wananchi.

"DC (Mkuu wa Wilaya) ni mgeni lakini ameshaligundua tatizo lililopo kwenye kata hii, leo mheshimiwa RC tulikuwa tumejiandaa utuchape maana utekelezaji wa miradi kwenye kata hii kasi yake siyo kubwa kwa sababu ya diwani kuwashawishi wananchi kugoma," alisema.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Wilaya ya Manyoni, Barnabas Mushi, alisema CCM inafahamu matatizo ya diwani huyo ambaye ana misuguano na watu wa eneo lake na chama kinaendelea kulifanyia kazi ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Diwani wa Kata ya Mitundu, Masanja akijibu tuhuma hizo alisema syio za kweli, hawezi kuhamasisha wananchi wagomee kushiriki nguvu kazi. Alisema mikutano iliyofanyika ya viongozi wa wilaya wa chama na serikali hakuweza kuhudhuria kwa sababu alikuwa amekamatwa na kuwekwa ndani.

Kutokana na hali hiyo, Serukamba alimtaka diwani huyo kubadilika na kuacha tabia hiyo.

Alisema serikali imeleta mamilioni ya fedha kwenye kata hiyo ili miradi itekelezwe na kukamilika kwa wakati kwa kushirikiana na wananchi.

Serukamba alisema: "Diwani naomba ubadilike usipambane na watu, kwenye siasa ukitaka kufanikiwa usipambane na watu maana wananchi ndiyo mabosi wetu, ukipambana nao kwanza hawatajitokeza kwenye kazi zako na pili utaishi maisha magumu ya kisiasa, haiwezekani watu wote wakuseme wewe tu itakuwa kuna tatizo".





# TARI yaanza mkakati kufufua kilimo cha ulezi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, kimeanza kufufua kilimo cha ulezi kwa kufanya utafiti na kuzalisha mbegu mbalimbali za zao hilo, kuzisambaza kwa wakulima kwa lengo la kuimarisha uchumi.

Pia imeanza kuhamasisha wananchi kulima zao hilo ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yamekuwa yakiathiri uzalishaji wa mazao mengine hasa uhaba wa mvua kutokana na zao hilo kuvumilia ukame. Mwishoni mwa wiki taasisi hiyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo wakulima na wafanyabiashara wa ulezi iliadhimisha Siku Maalumu ya Ulezi ambayo imeanzishwa na taasisi hiyo kwa lengo la kuhamasisha kilimo cha zao hilo.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Dk. Denis Tippe alisema taasisi hiyo imekamilisha utafiti wa mbegu za aina tatu na imeanza kuzisambaza kwa wakulima.

Alisema ulezi ni miongoni mwa mazao ambayo taasisi hiyo imeyafanya kuwa ya mkakati kutokana na kuwa na faida mbalimbali kwa wakulima na kwa watumiaji wa bidhaa zinazozalishwa kutokana na zao hilo hasa vyakula.

Alisema ulezi unastawi katika maeneo yenye mvua kidogo, hivyo akawashauri wananchi kuchangamkia kilimo cha zao hilo ili kujiongezea kipato.

"Ulezi una faida kiafya kwa sababu una madini mengi ya zinki, chuma, kasham na kiwango kikubwa cha wanga ikilinganishwa na nafaka zingine, kwa hiyo tunawashauri wananchi kutumia zao hili ili kuondokana na tatizo la udumavu hasa kwa watoto," alisema Dk. Tippe.

Alisema katika harakati za kulifufua zao hilo wametafuta mbegu mbalimbali za asili kutoka maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kuzifanyia utafiti wa vinasaba ili kupata mbegu ambazo zitafaa kuzalishwa katika maeneo yenye hali ya hewa tofauti.

Baadhi ya wadau walioshiriki maadhimisho hayo walisema zao hilo lilikuwa limeanza kupotea kutokana na wakulima kutojua umuhimu wake na hivyo kuanza kuzalisha mazao mengine tofauti.

Adam Mwakatumbula ambaye ni Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Nafaka katika Soko la Mwanjelwa jijini Mbeya, alisema miaka ya nyuma zao hilo lilikuwa linapatikana kirahisi kutokana na wakulima kuwa wengi lakini miaka ya karibuni limekuwa adimu.

Alisema kwa sasa wazalishaji wengi wa zao hilo wapo katika Mkoa wa Rukwa lakini kwa Mkoa wa Mbeya ni wachache na hivyo huwa wanalazimika kusafirisha kutoka Rukwa.

Alisema awali walikuwa wanajua kwamba ulezi ni kwa ajili ya kutengeneza uji na ugali pekee lakini kupitia TARI Uyole wamefundishwa kwamba zipo bidhaa zingine zinazozalishwa kwa kutumia zao hilo.

Alisema baadhi ya bidhaa hizo ni supu na keki na kwamba walibaini kuwa zao hilo lina faida kubwa kuliko mazao mengine ya nafaka ambayo wamekuwa wakiyatumia.

"Kwa sasa kilo moja ya ulezi tunauza Sh. 4,000 na hakuna nafaka nyingine ambayo bei yake ni kubwa kiasi hicho, tunawaomba hawa wataalamu waendelee kufanya utafiti wa hili zao ili wakulima wengi zaidi waanze kuzalisha," alisema Mwakatumbula.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malissa ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo aliwapongeza wataalamu wa TARI kwa kulifanyia utafiti wa zao hilo muhimu.

Hivyo, aliwataka watafiti kuendelea kusambaza mbegu hizo pamoja na teknolojia mbalimbali za uzalishaji kwa wananchi ili waanze kuongeza uzalishaji kwa lengo la kuimarisha uchumi wao na usalama wa chakula.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malissa (kushoto), akipata maelezo kuhusu uzalishaji wa mbegu za ulezi kutoka kwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, Dk. Denis Tippe (wa pili kushoto), katika maadhimisho ya Siku ya Mkulima wa Ulezi yaliyofanyika kwenye mashamba ya kuzalishia mbegu ya kituo hicho mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Serikali yawatangazia kiama watoroshaji tumbaku

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya imewatahadharisha wakulima na wanunuzi wa tumbaku watakaodiriki kutorosha zao hilo kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani. Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Saimon Mayeka, alitoa tahadhari hiyo juzi kikao cha wadau wa tumbaku kilichokuwa na lengo la kufanya tathmini ya uzalishaji wa zao hilo katika msimu uliopita na maandalizi ya msimu ujao.

Kikao hicho kiliitishwa na Chama Kikuu cha Wakulima wa Tumbaku wilayani humo (CHUTCU) na kuwashirikisha wadau mbalimbali wa kilimo zikiwamo taasisi za kifedha, wakulima, wasambazaji wa pembejeo za kilimo na maofisa wa kampuni zinazonunua zao hilo.

Alisema mbali na kuwafikisha mahakamani tumbaku itakayokamatwa itataifishwa pamoja na chombo kitakachokutwa kinatumika kwenye usafirishaji huo.

Hivyo, alizitaka kampuni zinazonunua tumbaku kwa wakulima kuwalipa fedha zao kulingana na madaraja na kwamba lazima ziwalipe mapema ili wafanye maandalizi ya msimu mwingine.

"Kampuni zinatakiwa kununua tumbaku ya wakulima kwa bei nzuri kulingana na madaraja, lakini zikishanunua ni marufuku mtu yeyote kutorosha tumbaku, ni lazima biashara ifanyike kwenye mfumo wa ushirika," alisema Mayeka.

Katika hatua nyingine Mayeka aliwataka wakulima wilayani humo kujiunga na bima za mazao ili wafidiwe endapo mazao yao yatakumbwa na majanga mbalimbali ikiwamo mvua na ukame.

Meneja Mkuu wa CHUTCU, Christian Msigwa alisema katika msimu wa kilimo uliopita baadhi ya wakulima walikuwa wanachanganya tumbaku na wengine walikuwa wanamwagilia maji ili kuongeza uzito jambo ambalo lilikuwa linaharibu soko.

# Wanafunzi 200 watumia darasa moja Mbalizi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Nsalala iliyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wanalazimika kukaa zaidi ya 200 kwenye darasa moja kutokana na uhaba wa vyumba hivyo.

Hayo yalisemwa na walimu wa shule hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya, iliyolenga kukagua mradi wa ujenzi wa vyumba 16 vya madarasa kwenye shule hiyo kupitia mradi wa 'bust'.

Mradi huo unatajwa kwenda kutatua tatizo la uhaba wa madarasa na hivyo kufanya wanafunzi kukaa 60 kwenye chumba kimoja tofauti na ilivyokuwa awali.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, John Malila alisema wanafunzi wamekuwa wakikaa kati ya 150 na 300 kwenye chumba kimoja hali ambayo inasababisha hata ufanisi wa ufundishaji kuwa mdogo.

Alisema walimu wamekuwa wakishindwa kuwafundisha vizuri kutokana na wanafunzi kurundikana kwenye chumba kimoja hali ambayo alisema huwa inaathiri hata ufaulu wa wanafunzi.

"Mradi huu utatusaidia kuboresha ufaulu wa wanafunzi wetu kwa sababu walimu watakuwa na nafasi ya kumfikia kila mwanafunzi kwa urahisi na hata wanafunzi watakuwa na uwezo wa kuwafikia walimu kwa haraka," alisema Mwalimu Malila.

Aliishukuru serikali kwa kuanzisha mradi huo kwa maelezo kuwa mrundikano wa wanafunzi kwenye vyumba vichache vilivyopo ulikuwa unahatarisha hata afya zao.

Baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo walisema wamekuwa wakishindwa kujisomea vizuri darasani kutokana na kurundikana wakieleza kuwa wakati mwingine hata hewa inakuwa haiwatoshi.

Mmoja wa wanafunzi hao, Shalom Njau aliishukuru serikali kwa kuwajengea madarasa hayo mapya akieleza kuwa shule zitakapokuwa zinafunguliwa hawatarundikana tena kwenye madarasa ya zamani.

Nao baadhi ya wananchi wa eneo hilo waliishukuru serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo wakieleza kuwa kwa kutumia michango yao kama ilivyokuwa zamani wasingeweza kufanikisha ujenzi huo.

Mmoja wa wananchi hao, Enock Mendagani alisema vyumba vya madarasa vinavyojengwa kwenye shule hiyo ni sawa na shule mpya wakisema kwamba vyumba 16 vinatosha hata shule ya sekondari.



## Vyama vya siasa vyawaita wanawake kugombea uongozi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VYAMA vya siasa nchini vimesema milango ipo wazi kwa wanawake kushiriki katika siasa ikiwamo kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika majimbo ya uchaguzi, kwamba hakuna vikwazo.

Hayo yalisemwa na Katibu wa Idara ya Itikadi na Uenezi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Khamis Mbeto Khamis, wakati akifungua mafunzo ya uongozi na siasa kwa wanawake wa vyama vya siasa wanaotarajia kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 yaliofanyika visiwani humo.

Mbeto alisema wanawake wameonesha uwezo mkubwa katika kuwania nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali kwa mafanikio makubwa ikiwamo kuanzia uwaziri hadi katika majimbo ya uchaguzi.

Alisema kwa upande wa CCM kwa muda mrefu imejenga misingi bora na imara ambayo imewawezesha wanawake kufikia dhamira za kisiasa za uongozi katika ngazi mbalimbali.

Alisema dunia imebadilika ambapo huu ni wakati muafaka kwa vyama vya siasa kutoa nafasi kwa wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi wa kisiasa ili kufikia malengo endelevu ya dunia ya wanawake na uongozi wa kijinsia.

"Chama Cha Mapinduzi siku zote kinawataka wanawake wasimame katika kuwania nafasi za uongozi na milango ipo wazi na hakuna vikwazo vya kuwazuwia,"alisema.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Salum Mwalimu, aliwataka wanawake wajitokeze kwa wingi kuwania nafasi za kisiasa katika majimbo ya uchaguzi na kuacha kulemazwa na nafasi za viti maalumu.

Alisema CHADEMA kilichukua juhudi za makusudi za kutoa nafasi za juu za uongozi katika majimbo ya uchaguzi kwa wanawake na kufanikiwa.

# Kasi usafirishaji watoto yamshtua Katibu Mkuu Maendeleo ya Jamii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Abeida Rashid Abdalla, amesema kuna wimbi la watoto kusafirishwa kwa ajili ya kufanya kazi za ndani na badala yake watoto hao hukumbana na vitendo vya udhalilishaji.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki visiwani Zanzibar wakati wa uwasilishaji wa taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa mpango kazi wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji mwaka 2017/2022.

Hivyo aliwataka wadau mbalimbali kuendelea kushirikiana na serikali kutokomeza vitendo vya udhalilishaji Zanzibar.

Alisema ushirikiano unahitajika kwasababu serikali pekee haiwezi kumaliza tatizo hilo, hivyo ushirikiano huo utasaidia kutokomeza janga hilo.

Abeda alisema vitendo hivyo vimekuwa vikiongezeka siku hadi siku hivyo inahitajika mkakati wa pamoja kuvimaliza.

Alisema hakuna sababu ya kunyamazia vitendo hivyo, lazima kupaza sauti huku akibainisha kwamba Mkoa wa Mjini Magharibi unaongoza kwa vitendo hivyo kwa Tanzania nzima.

Hivyo aliwataka wazazi na jamii kuwa makini na malezi ya watoto wao na kuwachunga katika matumizi ya mitandao ya kijamii kwasababu wengi wanaachiwa na kuchezea simu kuangalia vitu vya ovyo.

"Tunatakiwa kuzungumza mambo hayo kwenye jamii zetu labda watu watashtuka na kuacha katika mambo ya udhalilishaji," alisema.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa UN Women, Lucy Tesha, alisema mashirika hayo yataendelea kuunga mkono kuhakikisha vitendo hivyo vinatokomezwa.

Alisema kupitia tathmini hiyo ni fursa kwa wadau wote na serikali kujua kwa kiwango gani katika utekelezaji wa mkakati huo, mafanikio yake na matatizo yaliyopo na namna ya kuzifanyia kazi kwa lengo la kusonga mbele.

Wakati akiwasilisha tathmini hiyo, mshauri wa masuala hayo Massud Nassor, alisema tathmini inaonyesha vitendo hivyo vinaongezeka ikilinganishwa na mwaka 2016 mpango huo ulipoanza.

Kwa mujibu wa ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar kwa mwaka 2021 matukio 1,222 ya udhalilishaji yaliripotiwa Zanzibar, mwaka 2022 yalikuwa 1360 na kutoka Januari hadi Aprili mwaka huu matukio hayo ni 243.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na waumini wa dini ya Kiislamu baada ya kumalizika kwa kisomo cha hitima na dua ya kumwombea marehemu Sheikh Abubakar Said Alhashimy (Mwalimu Abuu) jijini Zanzibar mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima viungo waandaliwa mazingira ukuzaji kipato

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Mipango, Sera na Utafiti kutoka Wizara ya Kilimo, Maliasili na Umwagiliaji, Makame Kitwana Makame amesema Serikali ya Zanzibar inawathamini wakulima wa viungo ili wajikwamue na hali ya maisha na kukuza kipato chao.

Aliyasema hayo jana alipofanya ziara ya kuwatembelea wakulima wa mradi wa viungo visiwani humo akiongozana na wadau wa mradi huo wakiwemo Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA-Zanzibar) na wajumbe kutoka Jumuiya ya Ulaya (EU).

Alisema lengo la ziara hiyo ni kuangalia uendeshaji wa mradi huo unavyoendelea kwa wakulima ili kama kuna matatizo yanayowakabili yatatuliwe ili kuendelea na kilimo kama malengo ya mradi inavyotarajiwa.

Mkurugenzi huyo alisema serikali ni wasimamizi wakuu katika mradi huo kwa kuwapatia wakulima mafunzo na watalamu ili waendane na wakati, kupata mazao mengi.

Aidha alisema matatizo yaliyojitokeza ni mabadiliko ya hali ya hewa na ukosefu wa soko lakini serikali inaendelea kuifanyia ili wakulima wapate masoko ya uhakika ya kuuzia bidhaa zao wanazozalisha.

Naye mkulima wa viungo kutoka Kijiji cha Umbuji, Mrisho Suleiman Mwita, alisema kwa sasa hali ya kilimo cha vitungu imekuwa nzuri wakati huu wa mvua za masika na anatarajia kupata mavuno mazuri katika kilimo cha vanila.

Alisema kuwa elimu aliyopata kutoka kwa wataalamu wa mradi huo imempa uwezo wa kulima kilimo hicho kisasa zaidi na kutegemea kupata manufaa makubwa ya kiujuzi kufanya kazi hiyo kwa umakini.

Alisema licha ya kuwapo kwa mafanikio makubwa ya kilimo hicho lakini bado anakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa maji hasa wakati kipindi cha kiangazi ambapo kipindi hicho husababisha mimea kufa kwa jua kwa vile huduma ya maji hukosekana.

Aidha alisema pia wanakabiliwa na tatizo la uharibifu wa mazao yao kutokana na wakulima kuacha mifugo yao katika mashamba.

Naye Mratibu wa mradi huo, Ali juma said, alisema lengo la ziara hiyo ni kuwasikiliza wakulima hao namna wanavyoendelea na kilimo hicho ili kuleta tija.

Alisema wakiwa kati maeneo hayo wamebaini kuwa wakulima wapo vizuri katika kukiendeleza kilimo cha viungo licha ya changamoto za hali ya hewa za upatikanaji wa maji.

Ziara hiyo iliwahusisha wakulima wa vijiji vya Umbuji, Kizimbani, Mahonda na Donge visiwani Zanzibar.

# Mradi REGROW watumia bilioni 4/- kusaidia jamii

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WIZARA ya Maliasili na Utalii kupitia Mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW), umetumia Sh. bilioni 4.1 kwenye mpango wake wa kuisaidia jamii inayoishi pembezoni mwa Hifadhi za Taifa.

Hifadhi zinazozunguka vijiji hivyo ni pamoja na Ruaha, Mikumi, Udzungwa, Hifadhi ya Nyerere zamani ikijulikana Pori la Akiba la Selous na Msitu wa Asili wa Kilombero uliopo chini ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Naibu Msimamizi wa Mradi Regrow, Blanka Tengia, alisema hayo wakati akimkaribisha Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Rebeca Nsemwa, kufunga mafunzo ya uwezeshaji jamii na watendaji wa serikali za vijiji 45 vinavyopatikana na hifadhi za taifa za kipaumbele kutoka wilaya 10 nchini namna ya usimamizi na uendeshaji wa vikundi vya Benki Jamii (COCOBA).

Viongozi na watendaji wapatao 91 wa vijiji hivyo ni kutoka Wilaya ya Mbarali, Kilolo, Iringa, Chamwino, Mvomero, Kilosa, Kilombero, Morogoro, Kisarawe na Rufiji.

Tengia alisema Mradi wa Regrow, unatekelezwa katika maeneo ya kipaumbele katika hifadhi hizo wananchi wa vijiji hivyo kunufaika kiuchumi, utalii na shughuli mbadala za kiuchumi zisizo na madhara kimazingira.

Alisema, mradi huo unatekelezwa kwenye vipaumbele vinne na cha kwanza ni kuimarisha usimamizi wa maliasili kwa kujenga uwezo wa kuzisimamia na kuboresha miundombinu.

Alisema miundombinu itakayoboreshwa ni pamoja na barabara, viwanja vya ndege, malango ya kuingilia, maeneo ya mapumziko (picnic), vituo vya doria na tafiti na vituo vya taarifa za utalii.

Alitaja kipengele kingine cha pili ni cha uboreshaji na kuimarisha shughuli mbadala za kiuchumi kwa jamii.

Alisema kwenye kipengele hicho kinakusudia kuisaidia jamii inayoishi pembezoni mwa hifadhi hizo kunufaika kiuchumi na utalii au shughuli mbadala za kiuchumi zisizo na madhara kimazingira.

Alisema ni kuifanya jamii hiyo iondokane kutegemea shughuli za uwindaji haramu wanyamapori, uvunaji wa misitu na uharibifu wa mazingira.

Tengia alisema katika utekelezaji wa kipengele hicho, Mradi wa Regrow kwa awamu ya kwanza vijiji 15 vimenufaika chini ya mradi huo.

Alisema vijiji hivyo vimeanzisha vikundi vya Cocoba (sawa na vikoba) 162 vyenye wanachama hai 3,149 na vikundi 160 tayari vimepatiwa fedha mbegu (mtaji), Sh. 1,453,272, 934 kwa ajili ya kuendeleza benki jamii ya Cocoba.

Pia, alisema vikundi vya miradi 154 vimechagua miradi ambayo itawaweshwa kupatiwa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa miradi na Sh. 2,709,763,096 zitatumika kwa ajili ya miradi hiyo.

Alitaja katika kipengele hicho, wanafunzi 376 wamechaguliwa kufanya mafunzo ya masuala ya utunzaji wa mazingira kwa jamii, Village Game Scouts (VGS) na jumla ya Sh. 507,709,000 zimetumika hadi sasa kwa ajili ya wanafunzi hao.

"Mpango huo umehusisha wanafunzi 125 wameshahitimu mafunzo hayo na wengine 121 bado wapo mafunzoni," alisema Tengia.

Tengia alisema kuwa vijiji 61 vinanufaika na mradi huo, awamu ya pili umetekelezwa kwa vijiji 45 ambao ni watendaji wa serikali za vijiji, maofisa Maendeleo ya Jamii wa vijiji na wasimamizi wa mradi huo ngazi ya wilaya 10.

Alitaja kipengele kingine ni kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya maji Mto Ruaha Mkuu na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji ili kupunguza au kuondoa upotevu wa maji na kuimarisha mifumo ya umwagiliaji.

Tengia alisema, mradi huo utawezesha utengenezwaji wa kingo kwenye Mto Ruaha ili kupunguza uwezekano wa mto kukosa maji na wanyama kuteseka.

Alisema hadi Desemba 2022, Mradi wa Regrow, umetekelezwa kwa asilimia 46 na kwamba mikataba minane imesainiwa hivi karibuni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika hifadhi hizo za kipaumbele na kazi utaanza wakati wowote.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Nsemwa alisema sekta ya utalii inapewa kipaumbele kutokana na vivutio mbalimbali nchini. Alisema, serikali inatambua uwapo wa jamii zinazoishi jirani na maeneo ya hifadhi na umuhimu wa ushiriki wao katika kulinda na kuendeleza maliasili zilizopo katika maeneo hayo.

## AzamPesa kuinua uchumi nchini

**Na Halfani Chusi**

HUDUMA ya kifedha kupitia simu ya mkononi ya AzamPesa, iliyozinduliwa juzi imetajwa kuwa itaongeza ajira na kuinua uchumi wa nchi.

Mkuu wa Kitengo cha Mauzo na Masoko wa AzamPesa Tanzania, Gillian Rugumamu, alisema hayo alipozindua huduma hiyo, akisisitiza, itawawezesha wateja wake kutuma na kupokea bure.

Alisema huduma hiyo inayojulikana kama kuwa huru tuma pesa bure, itawawezesha wateja kutoka mitandao yote ya simu kujiunga na kutumia huduma hiyo.

Alifafanua kuwa huduma hiyo imekuja baada ya kuzingatia mahitaji ya wateja na wana imani kuwa promosheni hiyo itakuwa chachu kwa wale ambao sio wateja wake kuchangamkia na kuanza kunufaika na huduma hiyo aliyoitaja kuwa ni salama, rahisi na ya uhakika bila makato.

"AzamPesa, tumejiwekea mikakati ya kuendeleza huduma bora nchini na tumejikita zaidi katika kuongeza mawakala wetu, tunaendelea kuongeza kwa kufanya huduma hii iwe rahisi zaidi.

"Huduma hiyo itawezesha malipo mbalimbali, yakiwamo yale ya huduma za serikali ambayo wateja wanaweza kufanya malipo wakiwa mahali popote na kwa wakati mmoja, pia imeunganishwa na benki mbalimbali, ili kurahisisha wateja kufanya miamala ya kibenki," alisema Gillian.

**AzamPesa, tumejiwekea mikakati ya kuendeleza huduma bora nchini na tumejikita zaidi katika kuongeza mawakala wetu, tunaendelea kuongeza kwa kufanya huduma hii iwe rahisi zaidi.**




Meneja Mkuu wa Bodi ya Puma Energy Tanzania, Fatma Abdallah (kushoto) na Mwenyekiti wa Bodi wa kampuni hiyo, Dk. Selemani Majige (wa pili kushoto), wakikabidhi hundi ya mfano kwa wanahisa wa Puma Energy Tanzania, ambao ni Mkuu wa Puma Energy Africa, Fadi Mitri (kulia mwenye miwani), aliyewakilisha kampuni ya Puma Investments na Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu, katika hafla ya kukabidhi gawio kwa wanahisa wa kampuni iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walimu waiangukia TSC upandishwaji madaraja

**Na Devota Mwachang'a**

WALIMU wa sekondari na msingi Manispaa ya Kinondoni waliojiendeleza kielimu wameiomba Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), kushughulikia madai yao ya kupandishwa madaraja, wakilalamikia utaratibu wa ubadilishwaji wa muundo "re-categorization" kucheleweshwa.

Madai hayo yanahusisha walimu waliojiendeleza kielimu kutoka ngazi ya cheti hadi stashahada, astashahada na wengine hadi shahada kupewa muundo wanaodai ni kandamizi kwa madai wengi hawakuuomba, na waliouomba zaidi ya miaka mitano iliyopita hawakupewa kwa wakati hadi ilipofika 2021-2022 ndipo wakaona miundo mipya kwenye 'payrolls' bila kupewa barua za miundo hiyo.

Wakizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, walimu hao waliomba Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora awasaidie kulitatua suala lao kwa kuwa ofisi ya utumishi Kinondoni haitoi majibu ya kujitosheleza.

Marciane Erwin, mmoja wa walimu shule ya msingi akizungumza kwa niaba ya wenzake alisema: "Tulitumia gharama zetu na muda wetu kujisomesha, lakini sasa tunakandamizwa kwa kulazimishiwa vyeo ambavyo vinaathiri mtiririko wa kupanda madaraja yetu.

"Tumelitumikia daraja la mwisho kwa miaka mitatu hadi mitano ndiyo tunapewa miundo mipya wakati tulitegemea kupanda daraja ndipo tuombe au tupewe muundo mipya, huu muundo unatukandamiza sisi wa Kinondoni, wenzetu tulipokuwa nao darasani wamepandishwa cheo huko mikoani walipo."

"Tunaomba serikali iondoe sheria ya muundo, hii ni kandamizi kwa walimu, kama haiwezekekani turekebishiwe mishahara na hicho cheo cha muundo kibaki kama kilivyo cha zamani," alisisitiza.

Alisema ni nafuu kwa wale walimu wa ngazi ya cheti ambao wanaendelea kubadilishiwa viwango vya mshahara na kupandishwa madaraja, tofauti na waliojiendeleza kielimu hawathaminiwi, wanatamani wasingepoteza muda kujiendeleza kwani miongoni mwao wapo wanaokaribia kustaafu.

Mwalimu mwingine (hakutaka jina lake litajwe) alisema: "Hapa wilayani kuna ucheleweshwaji wa kubadilisha muundo kwa watumishi, mfano sisi walimu wa sekondari na msingi tuliomba mwaka 2019, lakini tumekuja kubadilishiwa 2021, wakati huohuo mwalimu anatakiwa apande daraja 2023, kwa hiyo kubadilishiwa muundo kumeathiri mabadiliko ya vyeo na ngazi ya mshahara, atalazimika kutumikia tena kwa miaka mitatu zaidi, hivyo atakuwa amekaa kwenye cheo hicho kwa miaka saba."

Msemaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Gerry Chami, alipoulizwa kuhusu madai hayo alisema muundo wa utumishi (re-categorization) unaotumika ni mmoja kwa watumishi wote, na kwamba mtu akijiendeleza kielimu akirudi lazima akae kwenye nafasi aliyokuwapo kwa miaka mitatu.

Alisema, zipo sababu nyingi za mtu kumaliza kipindi cha miaka mitatu baada ya kujiendeleza na kuendelea kusubiri kwa miaka mingine zaidi, na kwamba iwapo kuna mwalimu ana malalamiko anayo nafasi ya kumpigia simu yeye msemaji awasiliane naye moja kwa moja.

"Kabla ya mtumishi kupanda cheo ama mshahara, kinachoangaliwa ni suala la kukasimiwa kwa maana ya kwamba kuingizwa kwenye bajeti, akikasimiwa atapanda tu, anapowekwa kwenye Ikama lazima awe ameshakasimiwa," alifafanua Chami.

# NBC kufadhili wanafunzi 1,000 wa elimu ya ufundi

**Na Mary Geofrey**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) kupitia ushirikiano wake na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imetambulisha mpango wake wa ufadhili wa masomo ya ufundi stadi kwa vijana 1,000 kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

Kufanikisha mpango huo maalum ujulikanao kama 'NBC Wajibika Scholarships; benki hiyo imetenga Sh. milioni 100 kusaidia ufadhili kwa wanafunzi hao katika vituo mbalimbali vya VETA nchini.

Hafla ya utambulisho wa mpango huo ilifanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ikiongozwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda, Mkurugenzi wa VETA Kanda ya Dar es Salaam, Angelus Ngonyani na maofisa waandamizi wa benki hiyo wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi.

Akizungumzia mpango huo, Prof. Mkenda aliitaja hatua hiyo ni mwitikio wa ombi lililowasilishwa kwa benki hiyo na serikali kupitia wizara hiyo baada ya kubaini kwamba licha ya serikali kuondoa ada katika masomo ya elimu ya msingi na sekondari, bado baadhi ya familia zimeshindwa kuwaendeleza kimasomo vijana wao kutokana na kukosa uwezo wa kifedha.

"Tunashukuru sana Benki ya NBC kwa kukubali ombi letu na leo hii kwa pamoja tunatambulisha mpango huu. Hatua hii inathibitisha dhamira sahihi ya benki katika kuisadia jamii inayoihudumia. Tunashukuru na hongereni sana," alipongeza.

Prof. Mkenda alibainisha kuwa kwa sasa serikali ipo katika utekelezaji wa mpango wake wa ujenzo wa vyuo vya VETA 64 kwa wakati mmoja katika wilaya mbalimbali nchini ikiwamo mikoa ya Songwe, Njombe na Geita ambayo haikuwa na vyuo hivyo. Alisema lengo ni kukamilisha adhma yake ya kujenga vyuo hivyo nchi nzima ili kuongeza idadi ya vijana nchini watakaojiajiri kupitia ufundi stadi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Sabi, alisema mpango huo unahusisha ufadhili wa masomo mbalimbali ya ufundi kupitia VETA ikiwamo ushonaji, useremala, ufundi magari, ujenzi, upambaji na mengineyo.

"Zaidi ya ufadhili wa masomo, benki pia itawaingiza vijana hao 1,000 katika mpango maalum wa elimu ya fedha ujulikanao kama 'NBC Business Club' na kuwafungulia akaunti maalum za 'NBC-KUA Nasi' zitakazowapa wasaa wa kutunza fedha bila gharama, kupata ushauri juu ya uwekezaji na kuwapa fursa za uwezeshaji kiuchumi kupitia mikopo ya kujiendeleza kibiashara," alisema.

Sabi alifafanua kuwa walengwa wa mpango huo ni vijana wenye umri kuanzia miaka 18 ambao wanatoka katika familia maskini.

Kwa mujibu wa Sabi, changamoto ya ajira kwa vijana ni kubwa huku soko la ajira rasmi likishindwa kumudu wingi wa vijana wanaohitaji ajira, hivyo suluhisho ni kuwatengenezea mazingira bora ya kujiajiri kupitia fursa zilizopo kupitia ufundi stadi, teknolojia na ubunifu.

"Kwa mujibu wa taarifa za Mtakwimu wa Serikali (NBS) mwaka 2018, nchi ilizalisha ajira rasmi 282,382 huku zaidi ya vijana 800,000 mpaka 1,00,000 wakiingia sokoni kusaka ajira.

Sabi alitumia fursa hiyo pia kutambulisha huduma mpya ya benki hiyo inayofahamika kama 'Akaunti ya Mwalimu' iliyoundwa mahusus kukidhi mahitaji ya kibenki ya mwalimu.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Sophia Jongo (wa pili kushoto), akipokea taulo za kike kutoka kwa Ofisa Uhusiano wa Jamii wa GGML, Ruth Mharagi (wa tatu kulia) hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni GGML ilivyojitosa kuimarisha usafi wa hedhi

**Na Halfani Chusi**

HEDHI ni sehemu ya maisha ya kawaida na yenye afya, lakini kwa wasichana wengi wanaopata hedhi, ni chanzo cha aibu, hofu na ubaguzi.

Ukosefu wa upatikanaji wa bidhaa za kutosha za hedhi safi na salama na elimu ya afya ya uzazi kwa wasichana na hata wazazi, kuna madhara makubwa kwa afya ya binti, elimu yake na hata maisha yake.

Kwa ujumla, afya duni ya hedhi na usafi hudhoofisha haki za kimsingi ikiwa ni pamoja na haki ya kufanya kazi, haki ya kupata elimu. Hali hii pia inazidisha ukosefu wa usawa wa kijamii na kiuchumi.

Ni kwa sababu hiyo Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) inayothamini maendeleo endelevu kwa jamii, inachukua hatua kusaidia mipango ya hedhi safi na salama katika jamii inayozunguka migodi yake.

Akizungumzia jitihada za kampuni hiyo katika kuboresha mazingira ya upatikanaji wa taulo za kike kwa wasichana, Meneja Mwandamizi wa GGML anayeshughulikia uhusiano, Gilbert Mworia, anasema wanaamini kwa kuboresha mazingira ya hedhi safi na salama, wanaweza pia kuwawezesha wanawake na wasichana na kupunguza unyanyapaa na ubaguzi na kuchangia katika kufikiwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

"Ndio maana katika maadhimisho Siku ya Hedhi Safi na Salama Duniani, ambayo huadhimishwa tarehe 28 Mei kila mwaka, GGML tuliandaa mfululizo wa shughuli za kuongeza uelewa na kutatua changamoto zinazohusiana na usafi wa hedhi.

"Mojawapo ya matukio hayo ilikuwa ni ziara ya kutembelea Shule ya Sekondari ya Wasichana Nyankumbu ambako wadau mbalimbali waliounganа na GGML walizungumza na mamia ya wanafunzi kuhusu suala hilo muhimu," anasema.

Ofisa huyo anasema GGML ilimwalika mtoa huduma za afya kueleza vipengele vya kibaiolojia na kisaikolojia vya hedhi na usafi sahihi wa hedhi. GGML pia ilisambaza masanduku 72 ya taulo za kike kwa wanafunzi na kuwaonyesha jinsi ya kuzitumia ipasavyo.

28 Mei mwaka huu, GGML iliandaa mkutano wa hadhara na Halmashauri ya Mji wa Geita kuadhimisha Siku ya Usafi wa Hedhi Duniani mkoani Geita. Mkutano huo ulihudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa serikali za mitaa, asasi za kiraia, vyombo vya habari na wanajamii.

Lengo la mkutano huo ni kueneza ujumbe kwamba hedhi safi ni suala la haki za binadamu, si suala la afya tu, kila anayepata hedhi anastahili heshima na utu.

"GGML inajivunia kuwa sehemu ya vuguvugu hili la kimataifa la kuvunja ukimya juu ya usafi wa hedhi na kuweka mazingira shirikishi zaidi na yenye msaada kwa watu wanaopata hedhi.

"Tunatumaini juhudi zetu zitawatia moyo wengine kujiunga nasi na kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya mamilioni ya wanawake na wasichana kote ulimwenguni," anasema.

Akizungumzia jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na shule hiyo ya wasichana Nyankumbu, Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Georgia Mugashe, anasema suala la hedhi safi na salama ni kipaumbele ambacho kimewekewa mazingira salama katika kila eneo la shule hiyo.

Akianza na elimu, Mwalimu Mugashe anasema huwapa wanafunzi wa shule hiyo elimu kuhusu afya ya uzazi kila mara na kuwafundisha namna ya kuchukua tahadhari.

"Kila mahali tumeweka taulo za kike, mabwenini wanazo, kama wapo shuleni kuna chumba maalum cha wasichana ambacho kimewekwa taulo za kike na miundombinu yake.

"Zingine zimewekwa kwa daktari au nesi katika zahanati iliyopo karibu na shule hii... kwa hiyo hata kama mwanafunzi anaumwa tumbo, akienda hospitali anapatiwa tauli za kike bure. Kwa hiyo kila mazingira ya karibu anapewa huduma hii bila malipo," anasema.

Mwalimu huyo anasema elimu hiyo kuhusu hedhi safi na salama inatolewa kwa ngazi zote ikianzia shuleni kwa wanafunzi kwa kushirikiana na halmashauri hata kwa wanafunzi wa shule nyingine lakini pia wanawashirikisha wazazi.

Mwalimu Mkuu huyo anaishukuru Kampuni ya GGML kwa kuendeleza juhudi za kuwasaidia wanafunzi na jamii inayozunguka mgodi huo vifaa mbalimbali ikiwamo taulo za kike ambazo zimeendelea kuwa mkombozi kwa watoto wa shule hiyo na hata kupunguza gharama za uendeshaji wa shule.

Maadhimisho ya Siku ya Hedhi Duniani mwaka huu yalikuwa na kaulimbiu ya kitaifa isemayo 'Hedhi ni tunu na msingi wa afya kwa wasichana na wanawake, tuiwezeshe'.

Ni kaulimbiu iliyolenga kuendelea kuweka mkazo katika masuala ya hedhi iliyo salama kwa wasichana na kinamama kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

# AZAM FC YAMGEUKIA KIPA GEITA GOLD

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kumsajili kiungo Feisal Salum 'Feitoto' kutokea Yanga, mabosi wa Azam FC sasa wanapambana kuhakikisha wanamsajili golikipa wa Geita Gold, Arakaza Macarthur raia wa Burundi ili kuimarisha kikosi chao kwa ajili ya msimu ujao wa ligi kuu na mshindano ya kimataifa.

**Golikipa huyo mkataba wake na Geita Gold unaelekea ukingoni na viongozi wa Geita wanapambana kutaka kumbakisha licha ya nia ya Azam ya kumtaka Mrundi huyo.**

Habari za uhakika zinaeleza Azam tayari wameshafanya mazungumzo na kipa huyo ambaye ameonyesha nia ya kutaka kujiunga na timu hiyo licha ya mabosi wake kupambana katika kuhakikisha anabakia kwa ajili ya msimu ujao.

"Ni kweli Arakaza anatakiwa na Azam kutokana na kiwango chake ambacho amekionyesha msimu huu, lakini hata Geita wenyewe kwa sasa wanamekuwa wakipambana kuhakikisha anabakia kwenye timu yao ili kuweza kutimiza malengo yao ya kufanya vizuri msimu ujao," alisema mmoja wa watu wa karibu wa golikipa huyo.

Aidha, mtoa habari huyo alisema licha ya klabu hizo kupambana kutaka kumsajili, golikipa huyo pia ana ofa mbili kutoka mataifa ya kiarabu wanamtaka.

Hata hivyo kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Geita Gold FC, Leonard Bugomora, alisema wamesikia tetesi za kipa huyo kutakiwa na Azam, hata hivyo hawako tayari kupoteza wachezaji wao muhimu na kipa huyo ni mmoja wao.

Alisema kamati ya utendaji ya klabu hiyo itakutana siku yoyote kuanzia sasa kufanya tathmini ya ligi iliyomalizika na kujadili mipango ya msimu ujao wa 2023/24.

"Tunatarajia kukutana kamati ya utendaji kupitia ripoti ya benchi la ufundi na kuona wachezaji ambao wamemaliza mikataba yao kuongezewa hasa wale waliokuwa kikosi cha kwanza, tunahitaji kuimarisha timu yetu, tunatambua kuna baadhi ya wachezaji wetu wa-



nawindwa na baadhi ya klabu akiwamo huyo kipa wetu (Arakaza), tunaamini tutawabakisha," alisema Bugomora.

Aliongeza kuwa baada ya kamati ya utendaji kukutana na kujadiliana mambo mbalimbali ikiwamo tathmini ya kikosi cha timu yao na wafanye nini kwa msimu ujao watawasilisha kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya timu hiyo.




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Dk. Pindi Chana (katikati), akiwa pamoja wachezaji na viongozi wa Timu ya Taifa ya Olimpiki maalumu baada ya kuwakabidhi Bendera ya Taifa jijini Dar es Salaam jana, timu hiyo inaenda kushiriki mashindano ya dunia yatakayofanyika Berlin, Ujerumani kuanzia Juni 17-25. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# KMC yatua Mbeya 'kujitafuta' Play Off

**Na Abdallah Mataka**

KIKOSI cha timu ya KMC tayari kimewasili jijini Mbeya kwa ajili ya mchezo wao wa kwanza wa mchujo "Play Off" dhidi ya wenyeji Mbeya City utakaopchezwa kesho kwenye Uwanja wa Sokoine.

KMC imetua Mbeya ikitokea Sumbawanga ilipoenda kucheza mchezo wao wa mwisho wa ligi kuu dhidi ya wapinzani wao hao ambapo waliibuka na ushindi wa bao 1-0 ushindi ambao hata hivyo haukuwasaidia kukwepa kucheza mchezo huo wa mchujo.

Akizungumza na Nipashe, ofisa habari wa klabu hiyo, Christina Mwagala alisema maandalizi kuelekea mchezo huo yanakwenda vizuri na wachezaji wote wapo katika hali nzuri kuelekea kwenye mchezo huo muhimu.

"Tunafahamu hatupo kwenye hali nzuri kujihakikishia kubaki ligi kuu msimu ujao, mchezo huu ni muhimu na wachezaji wetu wanatambua, kila mmoja akili ameelekeza kwenye mchezo huu kwa sababu hatutaki kushuka daraja," alisema Christina.

Aidha, Christina amewaomba mashabiki wa timu hiyo kuendelea kushirikiana nao katika kipindi hiki kibaya lakini ana imani wao kama KMC watafanikiwa kubaki Ligi Kuu msimu ujao.

KMC imemaliza Ligi Kuu ikiwa katika nafasi ya 13 baada ya kujikusanyia pointi 32 ikiwa ni pointi moja zaidi ya Mbeya City iliyomaliza katika nafasi ya 14.

Timu itakayofungwa kwenye matokeo ya jumla baada ya michezo miwili itashuka daraja moja kwa moja na itakayoshinda itakwenda kumenyana na Mashujaa FC ya ligi daraja la kwanza kuwania kucheza ligi kuu msimu ujao.

## Kocha wa Mfaume Mfaume atamba

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Bondia Mfaume Mfaume, Ramadhan Uadi 'Rama Jah' ametamba bondia wake kumpiga mpinzani wake Nkululeko Mhlongo wa Afrika Kusini na mashabiki waamue ampige raundi ya ngapi.

Rama Jah ametoa kauli hiyo ya tambo ikiwa ni wiki chache kabla ya pambano hilo lililopewa jina la 'Hata usipolala Patakucha tu' litakalofanyika Mlimani City jijini Dar es Salaam Juni 30.

Alisema wamejiandaa vizuri na wanaendelea na maandalizi kuelekea kwenye pambano hilo ambapo licha ya kutomdharau mpinzani huyo, bado ana uhakika bondia wake ataibuka na ushindi.

"Binafsi niwaachie mashabiki waamue Mfaume Mfaume ashinde kwenye raundi ya ngapi, tunamuheshimu mpinzani wetu kutokana na rekodi zake lakini bado kwenye mzani Mfaume Mfaume atashinda sina wasiwasi na hilo," alisema Rama Jah na kuongeza,

"Mpinzani tunamheshimu kwa rekodi yake na ubora wake, ana nyota mbili na nusu ni zaidi ya bondia wangu lakini nina uhakika wa ushindi," alisema.

## African Sports yashuka daraja, kucheza 'first league' msimu ujao

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa bao 1-0 iliyoupata African Sports juzi kwenye Uwanja wa Mkwakwani, Tanga dhidi ya TMA ya Arusha, haukuiwezesha timu hiyo kusalia Ligi ya daraja la kwanza 'Championship', badala yake imeshuka daraja na kwenda ligi daraja la pili 'first league'.

African Sports, Mabingwa wa Jamhuri ya Muungano Tanzania mwaka 1988, imeshuka daraja kwa kushindwa 'kupindua meza' ya matokeo ya mechi kwanza ya 'play off' iliyochezwa Juni 3 Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha ilipopokea kipigo cha mabao 4-0 na kufanya timu kuondolewa kwa jumla ya mabao 4-1.

Timu hiyo yenye maskani yake Tanga iliteremka miaka ya 1990, lakini ilifanikiwa kupanda tena Ligi Kuu msimu wa 2014/15, ikateremka 2015/16, kwenda 'Championship' na msimu huu imeshindwa kuhimili vishindo hadi kupelekwa kwenye 'play off', lakini huku nako imeshindwa kujitetea kubaki.

Matokeo hayo yanaifanya TMA kupanda daraja kutoka daraja la pili 'first league' na kwenda Ligi ya Championship na itaanza kucheza msimu ujao.

Mechi nyingine ya pili ya 'play off' inatarajiwa kupigwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam kati ya Dar City kutoka 'first league' na Green Warriors ya Ligi ya Championship.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MOUNT KIPAUMBELE MAN

KIUNGO wa kati wa Chelsea na England, Mason Mount mwenye umri wa miaka 24 ni "kipaumbele kikubwa" kwa Manchester United msimu huu, lakini klabu hiyo ya Old Trafford haitalipa zaidi ya pauni milioni 60 kumnunua. ***(Give Me Sport)***

### ATAKIWA NEWCASTLE UTD

KLABU ya Newcastle United ina nia ya kutoa "ofa kubwa" kwa kiungo wa RB Leipzig raia wa Hungary, Dominik Szoboszlai mwenye umri wa miaka 22. ***(L'Equipe, via Sport Witness)***

### MAN UNITED WASIWASI

MANCHESTER United ina wasiwasi mpango wao wa kumsajili beki wa Napoli raia wa Korea Kusini, Kim Min- jae mwenye umri wa miaka 26, unaweza usifaulu ikiwa Harry Maguire atakataa kuondoka Old Trafford. ***(90min)***

### RICE NA ARSENAL

ARSENAL inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili nahodha wa West Ham United, Declan Rice mwenye umri wa miaka 24, lakini bado haijajiandaa kukidhi bei inayotakiwa na wagonga nyundo hao kwa kiungo huyo wa kati wa England. ***(90min)***

### PALHINHA KUMRITHI RICE

KLABU ya West Ham inapanga kiungo wa kati wa Fulham na Ureno, Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 27 kama mbadala wa Declan Rice. ***(talkSPORT)***

### COSTA AWANIWA

KLABU ya Manchester United inajaribu kupunguza bei inayotakiwa kwa mlinda mlango wa kimataifa wa Ureno, Diogo Costa mwenye umri wa miaka 23, huku klabu yake ya Porto ikishikilia kwa euro milioni 75. ***(A Bola)***

### GYOKERES AGOMBEWA

KLABU ya Everton imejiunga na kinyang'anyiro cha kumnunua mshambuliaji wa Coventry raia wa Uswisi, Viktor Gyokeres, 25, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa West Ham, Wolves, Fulham, Leeds United, Southampton na Sporting Libson. ***(A Bola)***

### KONE AGOMBEWA

KIUNGO wa kati wa Borussia Monchengladbach aliyekadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 30, Manu Kone mwenye umri wa miaka 22, yuko kwenye orodha ya wanaowaniwa na Liverpool. ***(Sky Sports Germany, via Inside Futbol)***

### ADA YA FRIMPONG

KLABU ya Bayer Leverkusen inataka euro milioni 40 pamoja na nyongeza kwa beki wa Uholanzi, Jeremie Frimpong mwenye umri wa miaka 22 msimu huu, huku ada hiyo ikionekana kutokuwa na uhakika wa moja kwa moja wa kuwaondoa washindani wake waki-wamo Manchester United. ***(Metro)***

### ZANIOLO AWINDWA

KLABU za Aston Villa na Tottenham Hotspur zi-namwinda mshambuliaji wa Italia, Nicolo Zaniolo, 23, kutoka Galatasaray lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka Juventus na AC Milan kumnunua mchezaji huyo, ambaye ana kipengele cha kutolewa cha euro milioni 35. ***(Tuttojuve.com)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: UBINGWA WA MAN CITY UMEANDIKWA NA NYOTA

**ISTANBUL,** Uturuki

PEP Guardiola amesema taji la kwanza la Manchester City la Ligi ya Mabingwa Ulaya "limeandikwa na nyota" na ameipongeza klabu hiyo kwa kushikamana naye wakati wengine huenda wangemfukuza kwa kuchukua muda mrefu kuwa mabingwa wa Ulaya.

**Guardiola alinyanyua taji hilo mjini Istanbul nchini Uturuki Jumamosi baada ya ushindi wa 1-0 dhidi ya Inter Milan kwa bao la Rodri alilolifunga dakika ya 68.**

"Inter ni wazuri sana. Vuta subira, nilisema wakati wa mapumziko. Lazima uwe na bahati," Guardiola alisema.

"Iliandikwa katika nyota. Ni yetu."

"Kwanza kabisa maneno yangu ya kwanza ni kwa Inter, kuwapongeza kwa uchezaji wao," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

> ●●● Inter ni wazuri sana. Vuta subira, nilisema wakati wa mapumziko. Lazima uwe na...

"Jambo la pili ni kwa mkurugenzi wangu wa michezo, Mkurugenzi Mtendaji na mwenyekiti wangu, kwa kawaida usiposhinda Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya miaka mingi unafukuzwa.

"Moja ya sababu kubwa iliyofanya klabu hii iwe hapa tulipo ni watu kutoka Abu Dhabi. Sheikh Mansour bin Zayed Al Nahyan alichukua klabu na bila hilo tusingekuwa hapa. Ni watu muhimu zaidi.

"Wananiunga mkono bila masharti katika kushindwa katika shindano hili. Katika klabu nyingi hilo lingetokea na wewe unafukuzwa kwa hiyo ninatoa sifa ya ajabu kwa uongozi wangu kwa Mkurugenzi Mtendaji wangu."

Mafanikio katika Ligi ya Mabingwa Ulaya pia yalikamilisha mbio tatu za City baada ya kushinda pia taji la Ligi Kuu na Kombe la FA.

Na Guardiola alifichua kwamba Jumamosi asubuhi alipokea ujumbe kutoka kwa kocha wa zamani wa Manchester United, Sir Alex Ferguson ambaye aliiwezesha klabu hiyo kutwaa mataji matatu mwaka 1999.

"Ni heshima kwangu kuwa pamoja na Sir Alex Ferguson. Lazima niseme nimepata ujumbe kutoka kwake leo (juzi) asubuhi kwenye simu yangu ambao umenigusa sana."

Maswali kuhusu ni lini Guardiola angeshinda tena Ligi ya Mabingwa Ulaya yalikuwa yakimfuata kocha huyo mwenye umri wa miaka 52 tangu aliposhinda mara ya mwisho akiwa na Barcelona mwaka 2011.

Alikiri baada ya kuwashinda Inter ilikuwa "ahueni" kushinda tena lakini amesema sasa ana nia zaidi.

# PEREZ APANGA KUMSAJILI MBAPPE REAL MADRID




**MADRID,** Hispania

RAIS wa Klabu ya Real Madrid, Florentino Perez, amekiri kuwa anataka kumsajili Kylian Mbappe.

Forwadi huyo wa Ufaransa amekuwa akihusishwa mara kwa mara na kuhamia kwa Los Blancos hao tangu alipofanya vyema akiwa bado kijana mdogo kule AS Monaco.

Baada ya kuingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake mwaka 2021, Real Madrid ilitoa ofa ya wachezaji tisa kwa Paris Saint-Germain kwa ajili ya Mbappe mwishoni mwa dirisha la usajili la joto, lakini hilo lilikataliwa na miamba hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Ulimwengu wa soka ulitarajia hatimaye Mbappe angejiunga na Real Madrid mwishoni mwa msimu huo kwa uhamisho wa bila malipo, lakini katika hali ya kushangaza, alitia saini mkataba mpya Parc des Princes Mei 2022.

Lakini PSG ilishindwa kutamba kama washindani wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wa msimu wa 2022/23, na mapema kwenye kampeni Mbappe alikuwa tayari ameomba kuondoka kwa klabu hiyo. Huku PSG wakiwa tayari wamempoteza Lionel Messi kwa Inter Miami na Neymar pia huenda akaondoka - kwani Newcastle Unite wanamtafuta.

Real Madrid wenyewe wamempoteza mshambuliaji Karim Benzema kwa mabingwa wa Saudi Pro League Al-Ittihad na wanawinda nyota mpya, huku Harry Kane wa Tottenham Hotspurs akiwa miongoni mwa walengwa wao wakuu.

Video kwenye mitandao ya kijamii ilimwonesha Perez akiulizwa kama timu yake itamsajili Mbappe.

"Ndio, lakini sio mwaka huu," alijibu.

Real Madrid tayari wameanza biashara yao ya uhamisho wa majira ya joto kwa kumsajili beki wa kushoto Fran Garcia kutoka Rayo Vallecano, huku Brahim Diaz akisaini mkataba mpya baada ya kumalizika kwa mkopo wake AC Milan.

# Aston Villa wamsajili Tielemans wa Leicester

**LONDON,** England

KLABU ya Aston Villa imekubali dili la kumsajili mchezaji wa kimataifa wa Ubelgiji, Youri Tielemans kutoka Leicester City iliyoshuka daraja.

Villa imethibitisha kuwa kiungo huyo mwenye umri wa miaka 26 atajiunga nao Julai 1 baada ya miaka minne katika uwanja wa King Power.

Taarifa kwenye tovuti rasmi ya klabu ilisema: "Aston Villa ina furaha kutangaza kwamba klabu imefikia makubaliano ya kumsajili Youri Tielemans.

"Mchezaji wa kimataifa wa Ubelgiji, Youri Tielemans atakuwa Villan rasmi Julai 1 baada ya mkataba wake na Leicester City kumalizika."

Tielemans alijiunga na Leicester kutoka Monaco kwa mkataba wa pauni milioni 40 mnamo Julai 2019 baada ya kufanikiwa kwa mkopo katika kipindi cha pili cha msimu uliopita, baada ya kuanza kazi yake na Anderlecht.

Kwa jumla, aliichezea mechi 195 na kufunga mabao 28, likiwamo bao la ushindi walipoichapa Chelsea 1-0 kwenye fainali ya Kombe la FA 2021.

Pia aliwakilisha nchi yake kwenye fainali za Kombe la Dunia za 2018 na 2022 na Euro 2020.






# *William Saliba sasa ajifunga Arsenal*

**LONDON,** England

WILLIAM Saliba amekubali masharti ya mkataba mpya wa miaka minne na Arsenal, kwa mujibu wa ESPN.

Mkataba wa sasa wa beki huyo wa kati ulikuwa unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu ujao na baadhi ya timu maarufu barani Ulaya zilikuwa zimeanza kumwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ambaye mazungumzo yake na Arsenal kuhusu mkataba mpya yalianza tangu Septemba mwaka jana.

Saliba alikataa mapendekezo machache kutoka kwa Arsenal lakini haikueleweka kuwa alikuwa akishinikiza kuondoka kwa Washikabunduki hao na badala yake aliaminika kuwa anaangalia mpango ambao uliakisi hadhi yake kama mmoja wa walinzi bora chipukizi katika mchezo huo.

Wawakilishi wa Mfaransa huyo hivi majuzi walishinikiza kuongezwa kwa ofa na vyanzo vimethibitisha makubaliano yamefikiwa ya kuongeza mkataba wa Saliba hadi mwaka 2027.

Saliba amekuwa akitaka kusalia Arsenal, licha ya kuwindwa nchini kwao Ufaransa, na sasa anatazamiwa kuongeza muda wake wa kukaa Emirates.

Saliba alimaliza msimu wa 2022/23 akiwa na mechi 33 katika mashindano yote, mechi ya mwisho ilikuja Machi na shida ya mgongo iliyosababisha kampeni yake kumalizika ghafla.

Kikosi cha Mikel Arteta kiliteseka kwa kukosekana kwa Saliba, na kushinda mechi tano tu kati ya 11 za Ligi Kuu bila yeye na hatimaye kuangukia nyuma ya Manchester City katika mbio za ubingwa.

Arsenal tayari wamekamilisha mustakabali wa Gabriel Martinelli, Bukayo Saka na Aaron Ramsdale, na kumuunganisha Saliba kwenye mkataba mpya kutakuja kama nyongeza kubwa kwa mipango ya Arteta kwa klabu hiyo.

Winga Reiss Nelson pia inafahamika kuwa amekubali kuongeza muda wake kabla ya kumalizika kwa mkataba wake wa sasa msimu huu wa joto.

## Simba, Yanga U- 17 hakuna mbabe

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za vijana za Simba na Yanga chini ya miaka 17, juzi zilitoshana nguvu kwa kutoka sare ya bao 1-1, pambano la Ligi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF) chini ya miaka hiyo, inayoendelea kwenye viwanja wa Kituo cha Ufundi, Kigamboni, Dar es Salaam.

Katika pambano hilo mabao yote yalipatikana kwa mikwaju ya penalti, Simba ikianza kuandika bao mwanzoni mwa kipindi cha pili, tuta likifungwa na Zuberi Moshi, kabla ya Yanga kusawazisha mwishoni mwa mchezo kwa mkwaju wa penalti uliofungwa na Ahmed Mohamed.

Ligi hiyo ambayo inachezwa asubuhi na jioni, JKU Academy ililazimisha sare ya bao 1-1 Mbeya Kwanza, KMC ikaiangamiza Transit Camp mabao 5-2, JKT Tanzania ikaiadhibu Green Warriors mabao 2-1 huku Ruvu Shooting ikaibabua Pan African mabao 3-1.

Mechi zingine zilizochezwa Uwanja huo huo, African Lyon ilikung'utwa mabao 5-2 dhidi ya Karume Youth Centre.

Wakati huo huo, TFF imetangaza kikosi cha wachezaji 16 wa timu ya taifa ya soka la ufukweni inayotarajia kuingia kambini hivi karibuni kujiandaa na mashindano ya Afrika Tunisia, 2023.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya TFF, kikosi hicho kipo chini ya kocha Boniface Pawasa.

Wachezaji walioteuliwa wakiongozwa na Samson Mbangula wa Prisons, ni Shaaban Hassan Shaaban kutoka Ihefu, Adam Oseja, Juma Sultan, Jaruph Juma, wote wakiwa ni wachezaji huru, Ally Haji Juma wa JKU, Sadik Salim kutoka Green Warriors, Mtoro Nassor kutoka Msasani, Ismail Gambo wa KMC, Goodluck Gama wa Friends of Mkwajuni, Nuhu Ally wa Friends Rangers, Stephano Mapunda wa Mburahati, Yahaya Salmin wa Uhamiaji Zanzibar na Salum Mohamed wa Ilala.

## Robertinho

INATOKA UKURASA 24

Aidha, akizungumza na Nipashe jana mchana, Meneja wa Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alikiri Mbrazil huyo ameondoka kuelekea kwao kwa mapumziko huku akiwaachia majina ya wachezaji ambao hawahitaji kwenye kikosi chake cha msimu ujao.

" Ni kweli mwalimu amerejea kwao kwa ajili ya mapumziko lakini uongozi kwa sasa unajipanga kuanza kushusha vitu kwa ajili ya msimu ujao na hii imetokana na kushindwa kufanya vizuri katika michuano yote ambayo tumeshiriki msimu huu.

" Kikubwa ametuachia ripoti yake na nini ambacho anahitaji kwa ajili ya msimu ujao na kesho Jumatatu (leo) tunatarajia kuweka wazi kwa kuwatangaza nyota ambao tumewapa mkono wa kweli msimu huu," alisema Ahmed.

Aliongeza kuwa uongozi ulikuwa na vikao kwa wiki nzima na kikao cha jana kimehitimisha yale waliyojadili na kukubaliana kama bodi ya klabu.

Vikao hivyo vilikuwa chini ya Mwenyekiti wa Bodi, Salim Abdallah 'Try Again ', na wajumbe wote walihudhuria.

# NBC YAIPONGEZA YANGA UBINGWA, KUENDELEA KUDHAMINI LIGI KUU

**Na Mwandishi Wetu**

MDHAMINI Mkuu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Benki ya NBC imeipongeza klabu ya Yanga kwa kutwaa ubingwa msimu huu na kuahidi kuendelea kuidhamini ligi na kuifanya kuwa ya ushindani zaidi.

**Yanga Ijumaa iliyopita ilikabidhiwa rasmi kombe la ubingwa kwa msimu wa 2022/2023 baada ya mchezo wao wa mwisho dhidi ya Mbeya City kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.**

Benki hiyo imeahidi kuendelea kuongeza 'motisha' zaidi kwenye ligi sambamba na kubuni huduma mbalimbali za kibenki zinazolenga kuwasaidia wachezaji na wadau wengine wa mchezo huo ili kuwajengea uwezo wao pamoja vilabu vyao.

Akizungumza kwenye hafla ya kukabidhi kombe kwa Yanga iliyofanyika baada ya kukamilika kwa mchezo huo wa mwisho, Mkurugenzi wa Fedha wa NBC, Barnabas Waziri, aliahidi kuwa benki hiyo itaendelea kuwa mdhamini mkuu wa ligi hiyo na pia itaendelea kutoa mchango katika sekta ya michezo kwa upana wake.

"Katika msimu huu wa 2022/2023 Benki ya NBC tulifanya maboresho kadhaa ikiwamo kubuni huduma mbalimbali za kibenki zinazowalenga wachezaji na wadau wa ligi hii ikiwamo utoaji huduma ya bima kwa wachezaji wa ligi hii pamoja na familia zao pamoja na mikopo ya mabasi kwa vilabu vinavyoshiriki ligi. Pia tulikuwa tukitoa zawadi kwa wachezaji bora pamoja na kocha bora wa kila mwezi lengo likiwa ni kuongeza motisha na kuchochea ushindani," alisema Waziri.

Aidha, Waziri alisema anaipongeza Yanga kwa kufanikiwa kutwaa ubingwa msimu huu na hiyo ni furaha kwa mashabiki wa timu hiyo waliyoiunga mkono msimu wote.

"Udhamini wa NBC pamoja na wadau wengine kwenye ligi hii umesaidia sana kutatua changamoto kadhaa zilizokuwa zinapunguza ushindani kwenye ligi ikiwamo changamoto za kifedha, usafiri duni kwa baadhi ya timu na ukosefu wa huduma za afya ikiwemo bima za afya. Hatua hii imeongeza ushindani kwenye ligi na hiyo ndio sababu tunawapongeza sana Yanga FC kwa kuibuka washindi kwenye ligi hii ambayo ilikuwa na ushindani mkubwa," alipongeza.

Akikabidhi kombe hilo kwa Yanga SC, huku akishuhudiwa na maelfu ya mashabiki wapenda soka wa jiji la Mbeya na mikoa jirani ya Nyanda za Juu Kusini, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliishukuru Benki ya NBC kuwa mdhamini mkuu wa ligi hiyo huku akibainisha kuwa udhamini wa benki hiyo umekuwa na matokeo chanya kwa soka la Tanzania.

"Udhamini wa NBC umewezesha kuongeza ushindani kwenye ligi na kuboresha soka letu. Leo hii tunajivunia kuwa na ligi bora barani Afrika tukishikilia nafasi ya tano. Naipongeza sana benki ya NBC kwa kufanya mambo makubwa katika ligi na soka la nchi yetu kwa ujumla," alipongeza Homera.



Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya NBC, Waziri Barnabas (wa tatu kushoto), akiwa pamoja na wachezaji wa timu ya Yanga baada ya kukabidhiwa kombe la ubingwa wa Ligi Kuu kwa msimu 2022/2023 mwishoni mwa wiki jijini Mbeya. Wengine ni Mkuu wa Kitengo cha Masoko NBC, David Raymond (kulia) na maofisa wengine wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



# *Fainali bila Mayele, Aziz Ki*

INATOKA UKURASA 24

mengi na mechi ngumu hadi kufikia hapo, na kuongeza kuwa kila mechi ina mfumo wake, hivyo watacheza tofauti na walivyocheza dhidi ya Simba kwenye hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo.

"Kila kitu kipo tayari tumejiandaa na dakika 90 ndizo zitaamua," alisema Ongala na kuongeza,

"Ni mechi ambayo timu itakayoshinda tu itatwaa kombe, tayari tuna tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa, lakini kombe hili tunalitaka sana na litakuwa faraja baada ya kukosa ubingwa msimu huu," alisema Ongala.

Alisema wanaiheshimu Yanga kwa kuwa ndio mabingwa watetezi na mabingwa wa Ligi Kuu lakini kwake ni dakika 90 pekee ndizo zitaamua bingwa wa FA msimu huu.

# Michezo

Jumatatu Juni 12, 2023

Nipashe




Saliba ajifunga Arsenal UKURASA 22



DUBE

MUSONDA

## Robertinho auachia uongozi maagizo mawili

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho', ameondoka nchini juzi usiku kuelekea kwao Brazil kwa ajili ya mapumziko ya msimu baada ya msimu wa Ligi Kuu Bara kufikia tamati lakini amewaachia viongozi maagizo mawili aliyotaka yafanyiwe kazi haraka.

Robertinho ameutaka uongozi huo kwanza kufanya usajili kwa kufuata kile alichokieleza kwenye ripoti yake ambayo ameikabidhi kwa uongozi wa klabu hiyo.

Nipashe inafahamu maagizo hayo ni juu ya wachezaji anaowataka kusajiliwa na wale ambao ameomba waondolewe kwenye timu kwa kuwa hawatakuwapo kwenye mipango yake msimu ujao.

Mmoja wa wajumbe wa bodi wa klabu hiyo alisema jana jioni walikaa na kuanza kuipitia ripoti ya kocha huyo kwa lengola kuanza kuyafanyia kazi maagizo yake.

"Ni kweli ripoti ya kocha imefika na tumekutana katika kikao maalumu kuipitia na kuanza kuifanyia kazi, bodi imepania kuhakikisha timu inafanya vizuri msimu ujao na ndio maana tupo makini katika mchakato mzima wa usajili na uboreshaji wa kikosi chetu, alisema mjumbe huyo ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini.

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga fainali bila Mayele, Aziz Ki

## ●●● Azam yapania kulibeba kombe, Kaze asisitiza hakuna wa kuwazuia lakini...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa soka Tanzania Bara, Yanga, leo watashuka uwanjani kujaribu kukamilisha furaha ya msimu kwa kutwaa Kombe la Shirikisho (FA) watakapoumana na Azam FC huku ikikosa huduma za nyota wake, Fiston Mayele na Aziz Ki.

**Mayele ambaye amekuwa na msimu mzuri atakosekana kwenye mchezo wa leo baada ya kwenda kujiunga na timu yake ya taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo sawa na Aziz Ki aliyeenda kujiunga na timu yake ya taifa ya Burkina Faso.**

Mratibu wa timu hiyo, Hafidh Saleh aliiambia Nipashe jana kuwa licha ya juhudi za uongozi wa timu hiyo kuomba wachezaji hao wacheze mchezo wa leo ndipo waondoke, imeshindikana na kuwalazimu kuwaachia waondoke.

Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Congo ya Mayele wanatarajia kucheza na Gabon, Aziz Ki na timu yake ya Burkina Faso watacheza dhidi ya Cape Verde, mechi zote hizo zitachezwa Juni 18 kuwania kufuzu fainali za Afrika.

Mchezo wa leo ni fainali ya aina yake ambapo Yanga wanataka kukamilisha furaha ya msimu baada ya kutwa taji la Ligi Kuu na kufanikiwa kucheza fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika wakisubiri kuona kama watatwaa ubingwa wa FA.

Yanga itaingia kwenye mechi hiyo ikitaka kulitetea kwa mara ya pili kombe hilo, kwani ililichukua Julai 2, mwaka jana, kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid Arusha, ilipoifunga Coastal Union kwa mikwaju ya penalti 4-1, baada ya kushuhudia dakika 90 zikienda sare ya mabao 3-3.

Hata hivyo, Azam itataka kulichukua kombe hilo baada ya kushindwa kufanya hivyo kwa miaka mitatu iliyopita, mara ya mwisho ikiwa ni 2019, ilipoifunga Lipuli bao 1-0 la Obrey Chirwa katika mchezo wa fainali Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze amesema pamoja na kwamba timu zote zimepata nafasi ya kucheza mechi za kimataifa, lakini Yanga ni timu kubwa na kila mechi dhidi ya timu nyingine inakuwa na presha ya mashabiki, hivyo ni lazima wapambane ili kupata ushindi.

"Tunaingia uwanjani kwa kazi moja ya kusaka ushindi ili tupate kombe la pili msimu huu, tutawapa furaha mashabiki wetu na tumalize msimu wa mashindano vizuri," alisema Kaze.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Kally Ongala, alisema timu yake imepitia mambo

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >